Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 82 No. 236 | MUHAR.-SAF. 1444 AH | SEPTEMBA 2022 | IKHA 1401 HS | BEI TSH. 700/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na unapowaona wale wanaozihafifisha Aya Zetu, basi ujitenge nao mpaka wazungumze maneno mengine; na kama Shetani akikusahaulisha, basi usikae baada ya kukumbuka pamoja na watu wadhalimu. (AL-AN'AAM 6:69)

Makamu wa Rais Dkt Philip Mpango akutana na Waahmadiyya

Na **Mwandishi Wetu**

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango tarehe 15 Agosti 2022 amekutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania wakiongozwa na kaimu Amiri wa Jumuiya hiyo Sheikh Abdulrahaman Ame, mazungumzo yaliofanyika Ikulu Jijini Dar es salaam.

Katika mazungumzo hayo, Makamu wa Rais ameipongeza na kuishuuru Jumuiya hiyo kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali pamoja na kuiombea nchi na viongozi wake. Amesema Serikali inatambua mchango wa Jumuiya hiyo katika kutatua changamoto mbalimbali za wananchi hususani katika sekta ya afya, elimu, maji na nishati ya umeme.

Makamu wa Rais ameiasa taasisi hiyo pamoja na viongozi wengine wa dini kuweka mkazo katika kusimamia maadili hususani kwa vijana kutokana athari zitokanazo na mitandao ya kijamii hivi sasa. Pia amewasihi kuendelea kuhimiza waumini kufanya kazi ili kuleta maendeleo kwao na kwa taifa kwa ujumla. Makamu wa Rais amesema dini zinapaswa kuwa chanzo cha upendo na umoja baina ya Watanzania na hazipaswi kutumika kama chanzo cha chuki baina ya waumini.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akipokea zawadi ya QURAN TUKUFU kutoka kwa Kaimu Amiri wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania Sheikh Abdulrahaman Ame mara baada ya kumalizika kwa mazungumzo yaliofanyika Ikulu Jijini Dar es salaam leo tarehe 15 Agosti 2022.

Pia amewasihi viongozi hao kusisitiza waumini kushiriki katika zoezi la sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu. Amesema Serikali itaweza kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo pamoja na kufahamu namna ya kugawa rasilimali kama idadi ya watu na maisha yao itafahamika kupitia sensa.

Awali akitoa taarifa ya maendeleo ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania, Katibu wa Jumuiya hiyo Sheikh Seif Nakuchima ameishukuru Serikali kwa kuendelea kudumisha misingi ya amani pamoja na kutoa uhuru na kusimamia ili kila mwananchi aweze kutekeleza Imani yake pasipo kubughudhiwa.

Amesema Jumuiya hiyo inaendelea na kazi ya kuhamasisha amani hapa nchini ikiwemo kuanzisha siku ya waanzilishi wa dini ambayo imelenga kuchagiza amani pamoja na kuandaa mikutano inayolenga kuhimiza wananchi kuishi kwa amani, kuheshimiana na kuvumiliana kwa watu wa dini zote na jamii zote. Amesema katika mikutano hiyo hushirikisha viongozi wa Serikali, vyama vya siasa na vyombo vya usalama ili kuweza kuweka misingi imara ya amani katika maeneo husika.

Muharram

Na **Mwandishi Wetu**

"Hakika wale waliofarikisha dini yao na wakawa makundi-makundi, huna uhusiano nao wowote. Bila shaka shauri lao ni Kwa Allah; kisha Atawaambia yale waliyokuwa wakitenda."(6-160)



Hadhrat Abdullah bin Umr[ra]anahadithia ya kwamba Mjumbe wa Allah[saw] alisema; Umati wangu pia utakabiliana na hali zilizowatokea wana wa Israeli. Hali hizo zitafanana jinsi kiatu cha mguu mmoja kinavyofanana na kiatu cha mguu mwingine mpaka kama mmoja wao atakuwa amemzini mama yake, basi atatokea mtu mwenye bahati mbaya kama huyo katika umati wangu pia. Wana wa Israeli waligawanyika katika makundi sabini na mawili na umati wangu utagawanyika katika makundi sabini na tatu, na yote yataingia motoni isipokuwa kundi moja. Masahaba wakauliza; Kundi hili ni lipi? Mjumbe wa Allah[saw] akasema; Ni kundi ambalo watafuata sunna yangu na ya masahaba zangu'.

Hadhrat Masihe Ma`ud[as] alisema " Zama za Masihi aliyeahidiwa ambazo muradi wake ni karne ya 14 kuanzia mwanzo wake mpaka mwisho wake. Pia sehemu nyingine ya zama ambayo ni sawa na Khair-ul-Quruni na bora kuliko zama za Faij-e-A`waj. Hizi ni zama zilizobarikiwa ambazo fadhili na ukarimu wa Mungu umekadiria kuwa zama hizi zitawafanya watu waungane na masahaba. Utavuma upepo fulani kutoka mbinguni kwamba makundi haya sabini na tatu ya waislamu ambayo minghairi ya moja, yote ni doa baya kwa Islamu na yenye kuitia aibu chemchem hii tukufu, yataendelea kupungua yenyewe na makundi yote machafu ambayo yamo katika Islamu lakini yanakana uhakika wa Islamu, yatafutika duniani na hatimaye litabaki kundi moja tu ambalo watafuata nyayo za masahaba" (Tuhfa-e-Gholarwiyya,Uk, 227)

Jitahidini sana kumsalia Mtume[saw] katika mwezi wa Muharram.

Khalifa Mtukufu wa tano, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad aba alisema " Kuhusu kukubaliwa kwa maombi na Muharram, ningependa kueleza ya kwamba katika siku hizi, katika mwezi

Endelea uk. 9

Msikiti ndio Maskani!! uk. 3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Mpaka lini Afrika?

Yanakuwepo maswali mengi kuliko majibu toka Afrika ijipatie kile kinachoitwa uhuru wa bendera katika miaka ya sitini. Maswali yamekuwa mengi yakidhihirisha kuweweseka, maumivu makali, na kuona giza badala ya nuru katika mustakabali wa Afrika. Mwana historia maarufu wa Afrika amejaribu kuyakusanya maswali hayo.

Je kuwa na bendera zenye rangi nyingi na za kuvutia ndio uhuru tuliodai? Mizinga ishirini na moja wanayopigiwa viongozi wetu wanapokuwa nje ndiyo sababu iliyofanya watu washinde na njaa, waingie msituni, wafungwe, wengi kuachwa na vilema vya kudumu, ndilo hilo tulilolitafuta tulipopigania uhuru? Ilikuwa ni kutengeneza tabaka la kikundi cha watu wachache ambao hata bila ya kutuuliza wanafanya mambo eti kwa niaba yetu, wanaendesha magari ya kifahari wakati watoto vijijini na mijini wanateketea kwa utapiamlo? Ndio hilo hilo tulilolidai kwamba sisi tunaendelea kulima tusivyokula na kula tusivyolima? Mpaka lini Afrika? Majibu ya maswali hayo yanategemea uko katika tabaka gani. Je u miongoni mwa wale waliokaa mezani au miongoni mwa wale wanaosubiri makombo ili uokote? Kwa ujumla pamekuwepo na kilio, majuto, giza na kukata tamaa. Mwandishi mmoja maarufu wa Afrika Ngugi wa Thiong'o, yeye anasema; uhuru umetuletea viongozi wanaopenda kutembelea magari ya kifahari wakati wakulima wanashinda na kulala na njaa. Kwa ujumla hali si shwari Afrika. Rushwa imekithiri. Ukabila umetapakaa. Uhasama wa kidini umegusa kila pembe ya bara hili. Giza hilo limetanda na kila mtu analiona. La msingi sasa tunaliondoaje giza hilo. Tunaweza kufanya nini ili bara letu liweze kusonga mbele?

Wenye uchungu wametoa dawa ya matatizo yetu, lakini anayegusa kiini cha matatizo yetu ni Mtukufu Khalifa wa V Hadhrat Mirza Masroor Ahmad*atba*, ambaye anatuelekeza nini cha kufanya. Huzur anataka watu wa Afrika wajiamini, waonee fahari historia yao na bara lao. Mapenzi ya kuthamini historia yanasaidia kujiamini na kutoyumba. Wakati unapokea mambo kutoka kwa wengine yaje tu kusaidia na sio kubomoa misingi yako. Misingi yako haiwezi kujengwa na matofali ya nje. Ni muhimu matofali hayo yawe kutoka ndani. Huwezi kupandikiza mapinduzi kutoka nje. Mapinduzi ni matokeo ya harakati za ndani anasisitiza Huzur*atba*.

Akiendelea Huzur*atba* anafafanua; Mipango mizuri ya maendeleo ya nchi haiwezi kuwa kazi ya kundi Fulani, chama Fulani. Wananchi wote bila kujali itikadi zao na mtizamo washikirikishwe na watoe maoni. Ni unapojua kuwa hiki ni kitu changu, kimetokana na mimi ni hapo tu unapoweza kushiriki na kutoa mchango wenye manufaa kwa jamii. Kwa bahati mbaya ukoloni mahali popote ulipoweka mizizi ulijenga kasumba ya kuona vitu vya Serikali si vyako na wala huna sababu ya kuwa na uchungu navyo. Hii illikuwa sawasawa wakati wa ukoloni kwa sababu hiyo ilikuwa serikali ambayo haikupata ridhaa ya wananchi. Kuwa na fikra za namna hiyo ni kukosea sana. Mali ya Serikali ni mali yako, unatakiwa uitunze kama mboni ya jicho. Yule anayekosoa na kuonyesha njia mbadala asichukuliwe kuwa adui. Adui hajulikani kwa sura bali kwa vitendo.

Kuhusu taifa Huzur*atba* anasema; Haiwezekani taifa kujifanya kuwa kisiwa. Ni lazima kushirikiana na wengine. Ni lazima kufanya biashara na wengine ili nyote mpate faida na kunufaika. Kuwavutia wawekezaji ni njia ya kuleta maendeleo nchini ila panatakiwa uangalifu na uzalendo wa hali ya juu. Mwekezaji anahitaji urahisi wa kufanya shughuli zake usalama na utulivu wakati vyote hivi vinatolewa mwenyeji asisahau maslahi, utamaduni wake na vipaumbele. Na Waswahili husema mwamba ngoma huvutia kwake.

Yote haya yanawezekana kama kuna uaminifu. Kufanya kazi ukiwa unafahamu ya kwamba ulikula kiapo cha uaminifu katika kulitumikia taifa. Kila mmoja katika taifa anakula kiapo cha kuwa mwaminifu katika kutimiza wajibu wake. Viongozi wanaposhika vitabu vitakatifu na kuapa waelewe hiyo ni ahadi ya kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu. Wanapomalizia kiapo chao wanasema Mungu nisaidie. Sasa ujiulize Akusaidie katika nini? Je hayo unayoyatenda gizani unadhani Allah hayaoni?

Kupona kwa mataifa kutategemea ni kwa kiasi gani tunazingatia ushauri wa Khalifa wa zama. Watanzania sauti ya Khalifa wa Mwenyezi Mungu tumeisikia, lililobaki ni kuifanyia kazi.

Kweli ni Mapenzi ya Mungu

Na **Sh. Yusuf A. Kambaulaya**
Tabora

Allah Mtukufu baada ya kuumba ulimwengu, Akamtunuku mwanadamu akili zenye ufahamu ili tofauti ziwepo za utambuzi wa mambo ili baadaye mwanadamu aweze kuwajibika kwa Muumba wake, ilhali viumbe wengine kama vile Wanyama, wadudu, n.k. kwa sababu ya kutokuwa na akili na fahamu zenye utambuzi hawawajibiki kwa yeyote yule. Lakini mwanadamu kwa vile amepewa akili za ufahamu, ndio maana amepewa uhuru wa kuishi hapa duniani kwa utaratibu maalum.

Kwamba kwa vile amepewa ufahamu wa kujua baya na jema, basi yeye atalipwa ujira sawa na atakavyoishi kwa wema au kwa uasi. Ndiyo maana, Allah Mtukufu huwa Analeta Manabii wake duniani kutukumbusha sisi viumbe wake asili ya sababu ya sisi kuletwa hapa duniani. Manabii hawa wa Allah ni waonyaji na watoao Habari njema, huwasihi wanadamu waishi hapa duniani kwa wema, wapate malipo mem ana kama wataishi Maisha maovu watapata adhabu iliyoandaliwa kwa ajili ya wahalifu na waovu.

Mtume Muhammad*saw* ndiye Nabii wa Allah aliyepewa mafundisho yaliyokamilika kabisa kwa ajili ya wanadamu wote mpaka siku ya kiama. Na sawa na bishara za Masih Mauud*as* ameishadhihiri katika zama hizi kuendeleza kazi za Manabii kuwaita watu watende mema wapate radhi ya Allah waende peponi, na wakaidi bila shaka makao yao yatakuwa motoni – baada ya kukasirikiwa na Mola kutokana na maovu yao.

Hadhrat Masih Mauud baada ya kudhihiri akaanzisha Jamaat kwa amri ya Mwenyezi Mungu, Jamaat hiyo akaipa jina Ahmadiyya Muslim Jamaat. Yeye akaanzisha taratibu za kueneza ujumbe kwa watu. Akaanza kuandika vitabu na pia akaruhusu magazeti ya Jamaat yaanzishwe ili yasaidie kufikisha ujumbe wake sehemu mbalimbali na hasa katika nchi ya bara Hindi. Hivyo basi wakati wa uhai wake magazeti mawili yakaanzishwa katika lugha ya Kiurdu *AL FAZAL* na *AL HAKAM*. Na gazeti la Kiingereza likaanzishwa liliitwa *THE REVIEW OF RELIGIONS*. Haya yote yalianzishwa katika uhai wa Hadhrat Masih Mauud mwenyewe.

Maulana Sheikh Mubarak Ahmad alipoletwa Afrika Mashariki kuanzisha Jamaat Ahmadiyya, sawa na hali ilivyoruhusu, njia moja aliyoitumia kufanyia mahubiri ilikuwa ni uanzishwaji wa gazeti la Kiswahili akaliita *Mapenzi ya Mungu*, kuonyesha kuwa *Mapenzi ya Mungu* ndiyo kiini cha mahusiano mema baina ya watu duniani.

Gazeti la *Mapenzi ya Mungu* tangia kuanzishwa kwake 1936 limetumika kama silaha Madhubuti katika jihadi ya kutangaza utukufu wa Allah kwa mujibu wa mafundisho ya Islam. Gazeti la *Mapenzi ya Mungu* limetumika kama ngao ya kuelezea ubora wa mafundisho ya Islam ukilinganisha na mafundisho ya dini nyingine. Gazeti hili limekuwa ni ngao ya kukinga aina zote za mashambulizi dhidi ya utukufu wa Allah, dhidi ya Mitume wa Allah na hasa dhidi ya dini ya Islam na mwanzilishi wake Mtume Mtakatifu na Mbora wa Manabii yaani Mtume Muhammad*saw*.

Gazeti hili lilipoanzishwa mpaka leo limekuwa ni gazeti pekee la Kiislam linalotoa mafundisho sahihi ya Uislam. Gazeti hili lilianzishwa kuelimisha umma juu ya maelezo kamili na sahihi ya umoja wa Allah na ubora wa dini ya Islam. Gazeti hili lilianzishwa ili kutetea heshima ya Islam na ya Mtume Muhammad*saw* zilizokuwa zinachafuliwa na wafuasi wa dini ya Kikristo hasa viongozi wa Kanisa Katoliki. Viongozi hawa walitumia lugha chafu isiyokuwa na staha dhidi ya Muasisi wa Ahmadiyya Muslim Jamaat, Mirza Ghulam Ahmad*as* – Masih Mauud na Mahdi. Hii ilikuwa ni vita. Wapinzani wa Islam walikuwa wanaendeleza vita vya kidini kwa kueneza shutuma hizo waandishi wataalamu wanazuoni wa Kiislam wakiongozwa na Maulana Sheikh Mubarak Ahmad, alisaidiwa na Sheikh Amri Abedi Kaluta, Sheikh Jalaluddin Qamar, Sheikh Muhammad Munawwar, Sheikh Jamil ur Rahman Rafiq, Mwl Abdu Imran, Bw, Abdul Nasibu Hija, Mwl Mahmood Hamsin Mubiru na wengine ambao maandishi yao yenye elimu na hekima yakazifanya kalamu za wapinzani ziwe butu kwa kukosa hoja dhidi ya mashambulizi yao. Na hivyo gazeti la *Mapenzi ya Mungu* likawa ni darasa la kujielimisha juu ya mas'ala mbalimbali ya dini ya Islam na haja ya kujiongezea elimu na maarifa. Aidha tangia gazeti la *Mapenzi ya Mungu* lianzishwe limekuwa na hadhi kubwa ndani ya Makala na mashairi, kwani mashairi yanayochapishwa ndani ya gazeti hili *Mapenzi ya Mungu* hubeba jumbe za maarifa na maadili mema.

Gazeti hili lilitoa mchango mkubwa kabla na baada ya nchi ya Tanganyika kupata uhuru na baada ya nchi hizi mbili sasa ni Tanzania, na linaendelea kuwahamasisha wananchi wa nchi hii wathamini misingi ya kuendelea kuwa wema na wapendao haki na ukweli. Gazeti hili linaendelea kutoa mchango na kuhimiza maadili mema yazagazwe yenye kujenga mustakabali mwema kwa jamii ya wananchi wa nchi hii ya Tanzania na Afrika Mashariki, bali na Afrika nzima. Na kusema kweli ni kwamba gazeti hili la *Mapenzi ya Mungu* linaendelea kufanya kazi ile ile ya Manabii ya kuamrisha na kuhimiza mema na kuchangia kupiga vita maovu ya aina zote yanayozalisha fikra za kumuasi Allah na kwenda mbali naye. Maandishi yote yanayoandikwa ndani ya gazeti hili la *Mapenzi ya Mungu* kwa njia ya makala au mashairi yanazielekeza nyoyo za watu zijielekeze kwa Allah Muumba wa ulimwengu kwa kufanya ibada na kumkumbuka nyakati zote.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Msikiti ndio maskani



Na **Sheikh Karimuddin Shams**
Mbeya, Tanzania

Tunashuhudia kwamba wengi wa watu wamekuwa *busy* sana siku hizi na kila ukimuuliza anaonekana akishitaki kuwa na upungufu wa muda pamoja na kuwa na shughuli nyingi kisha wapo watu ambao hawana muda hata kwa ajili ya dhati yao na mara nyingi wanaonekana kuwa na matatizo mengi ya kifamilia ya kijamii kwa jumla na hii ndio hali yao halisi upande wa dunia ama upande wa dini nao hawana Habari hasa wakazi wa miji mikubwa mikubwa. Kwa kweli watu hao wamejipangia majukumu mengi ya ziada kama vile kukaa masaa na masaa kwenye mitendao mbali mbali ya kijamii ama vijana wanajishughulisha sana na michezo kwenye simu, laptop au play stations mbali mbali hadi wakina mama amabo huwa wanamajukumu mazito na makubwa ya kuwalea Watoto pia wanaonekana kutazama sana television au kucheza michezo kwenye tabs au simu ndio maana hawa watu wa namna hiyo wanashindwa kutekeleza vyema majukumu yao na ukweli usiofichika ndio huu kwamba watu hao wanajitaabisha wenyewe kwa sababu ya kutokupanga vizuri muda wao ama sisi watu wa dini tunapochunguza wakubwa wetu na wazee wetu wa zamani walikuwa na Maisha mazuri na matamu zaidi kuliko sisi si tu kwamba walikuwa hawana vitu hivi vya kupoteza muda bure bali walikuwa wamejishikilia sana na majukumu yao ya msingi kwa mfano walikuwa wanamkumbuka sana Mwenyezi Mungu na kuzoea kuenda msikitini Pamoja na kusikiliza mawaidha mazuri kisha walikuwa imara sana katika kuyafuata maagizo ya Allah^{swt} mfano wa Bwana wetu Mtume Muhammad^{saw} unapaswa kuushika hapo kwamba yeye alikuwa amezoea kuenda kufanya ibada ya Mwenyezi Mungu na kukaa sikuu kadhaa kwenye pango la Heraa akimkumbuka Mola wake na kumuabudu. Mama wetu wa waaminio bi Khadija^{ra} alikuwa anamuandalia masarufu ya siku kadhaa ya kuishi pangoni. Hebu tazameni kijana wa miaka 25 hivi aliyeoa karibuni anamuacha mke wake na kuenda kufanya ibada nje ya nyumba tena kwa masiku! Je, kuna mfano wa mtu mwingine yeyote unapatikana katika ulimwengu huu? Tunalazimika kukiri kwamba la hasha wallahi! Mfano huu haupo hata kwa manabii waliotumwa kabla yake.

Na mfano huu ni wa wakati alipokuwa baado hajajua kuwa u miongoni mwa manabi, wakati wa ujana ambapo vijana huwa na matamanio mengi ya hapa na pale ila baadaye alipojijua kuwa Nabii wa Allah na kiongozi wa ulimwengu wote akatuachia mifano mengi ya kuigwa na kwa sasa ningependa kuwakumbushia wasomaji wetu tukio moja tu ambalo limesimuliwa na bi Aisha mkewe^{ra} yeye anatusimulia kuwa *safari moja Mtume^{saw} alipoingia chumbani mwangu na baada ya kujulishana Habari aliniomba kwamba je ninamruhusu ili usiku wa leo apitishe kwenye Ibada nilmjibu ndio kwani furaha yangu ipo katika ridha yako ewe mjumbe wa Allah basi alienuka mara moja na kuanza kusali baada ya kupata udhu'u na alisali rakaa nne lakini msiniulize juu ya urefu na uzuri wa rakaa hizo kisha aliongeza rakaa nne tena wala usiniulize kuhusu urefu na uzuri wa rakaa hizo yaani alizirefusha mno Pamoja na kusali kwa uzuri wa hali ya juu kabisa halafu machozi yalikuwa yanatiririka machoni pake.* na katika riwaya nyingine bi Aisha^{ra} anaeleza kwamba *nilishuhudia kuwa miguu yake ilikuwa imevimba kwa sababu ya kusimama muda mrefu sehemu moja na anasema nilipomuuilza: "ewe mjumbe wa Allaha! Mwenyezi Mungu Ameshafuta madhambi yako yote sasa kwa nini unajitaabisha kwa kiasi hiki? Basi alijibu: Je Nisiwe miongoni mwa watumishi wake wanaomshukuru?"* (Sahih Bukhari, hadith na. 1130)

Ndugu wasomaji! Maneno hayo yanatakiwa yaandikwe kwa vino vya dhahabu kisha yanasomo kubwa mno kwetu sisi ambao tunaghafilika kufanya ibada ya lazima kabisa iliyofaradhi kwa nyakati tano. Vile vile tunapata kujua kwamba ibada ya lazima yaani sala tano ni chanzo cha msingi kwa ajili kumtolea shukrani Mwenyezi Mungu juu ya neema zake tunazozitumia kila wakati.

Historia inatueleza kuwa watu wengi walipatikana walioweza kujitenga na matamanio yao ya nafsi na kumuabudu Allah^{swt} lakini hawa wote walikuwa wafuasi wa Mtume Muhammad^{saw} walioiga mfano wa kipenzi cha Mwenyezi Mungu na fahari ya manabii wote.

Tunaposoma historia ya masahaba wa Mtume^{saw} tunapata kujua kuwa wao walikuwa wamezoea sana kusali na kushinda msikitini. Riwaya nyingi zinatuelezea kwamba masahaba wa Mtume^{saw} walikuwa wanasali katika msikiti moja kisha kuenda kusali sala hiyo hiyo tena kwenye msikiti mwingine.

Katika enzi tukufu ya Mtume wetu Muhammad^{saw} msikiti ulikuwa madrasa yao ya kuwalea waaminio kitabia na kikhulka na kuwaelimisha juu ya masuala mengi hata ya dunia. Mtume^{saw} alikuwa anakaa muda mrefu msikitini katika nyakati tofauti tofauti akiwajibu masahaba maswali yao ya kila namna na kuwahangakia maendeleo na mafanikio yao ya dini na ya dunia pia. Masahaba waliweza kujifunza kila walichkihitaji kutoka jukwaa la msikiti na watu hao hao waliokuwa wanashinda msikitini walipata mafanikio makubwa mno hata ya dunia na kuweza kushinda nusu ya dunia nzima kwa miaka kumi na miwili tu.

Kichwa cha Habari cha dhumuni langu la leo lina sema: اَلْمَسَاجِدُ مَكَانِيْ yaani *misikiti ndio maskani yangu*. Maneno haya ni ya Imamu wa Zama hizi Hadhrat Ahmad^{as} wala hayo si tamko tu bali yana uthibitisho wa hali ya juu kabisa. Riwaya zinatujulisha kwamba Hadhrat Ahmad^{as} alikuwa amezoea kushinda msikitini muda mwingi na kuzama kabisa katika ibada ya Allah^{swt} kwa kiasi hiki kwamba baadhi ya wakati watu, kwa sababu ya giza na kwa sababu Hadhrat Ahmad^{as} alikuwa hana mwili mkubwa walikuwa wanamfungia kwenye mikeka ya msikiti hali u ndani ya ibada.

Bwana mmoja anasimulia ya kuwa *safari moja ofisa fulani mkubwa wa serekali alimuuliza baba yake seyidna Ahmadas, nasikia unaye mtoto mwingine pia wakiume, mbona simwoni' mzee akajibu akicheka, " Ni kweli, nina kijana mwingine wa kiume, lakini hajitokezi sana nje, anakaa ndani tu kama bi arusi, kama unataka kumwona basi uende msikitini utamwona pembeni humo. Yeye daima hushinda mle mle msikitini wala hana haja ya kazi nyingine ya kidunia.* (Masihi Aliyeahidiwa uk.5-6)

Hadhrat Ahmad^{as} alikanyaga kweli kweli nyao za bwana wake Mtume Muhammad^{saw} na msikiti wake pia ukawa madrasa ya kuwalea waaminio wote na kuwaelimisha juu ya maswali yao ya kila namna. Riwaya zinatoa ushuhuda wa kutosha kabisa kwamba Seyidna Ahmad^{as} alikuwa na tabia ya kushinda msikitini na kukaa na masahaba akiwatolea majibu ya maswali yao na kuzungumza juu ya mambo yao mbali mbali. Kulikuwa na mahafali maalum kila siku baada ya sala ya magharibi na kipindi cha maswali na majibu kisha baada ya kufariki kwa Hadhrat Ahmad^{as} makhalifa wake wote waliendelea na mfumo huu huu wa kukaa na waaminio msikitini na kuwasikiliza shida zao na kuwaongoza hadi leo Waahmadiyya wanafaidika sana na uongozi wa Khalifa wetu wa tano Hadhrat Mirza Masroor Ahmad^{atba} na Waahmadiyya wanamuuliza juu ya shida zao na kujibiwa na majibu yatulizwayo hata wanafunzi wetu wanamwomba shauri lake juu ya kuchagua masomo yao ambayo yatawafanufaisha katika Maisha yao ya mbele n.k.

Ndugu wasomaji watukufu wa gazette la *Mapenzi ya Mungu*! Nimejaribu kuyaandika hayo yote ili tuweze kuunda mfumo wa aina hii na misikiti yetu yawe kisima cha elimu na amani kwa wote. Tuzoe kukaa msikitini na viongozi wetu wakiwemo walimu na masheikh na tujipatie malezi mema kwao, haya yote yanawezakana tu endapo tutakuwa na nia njema na adhma thabiti lakini kama tunashindwa kukaa kila siku basi angalau tupange siku za wiki endi yaani Jumamosi na Jumapili, tuwe tunashinda msikitini. Ninaamini kama tutapanga na kufanya hivyo basi mafanikio yatabusu miguu yetu. Ningependa kueleza pia kwamba wale Watoto wanaofika msikitini tusiwakaripie hata kidogo ili wapate kujijenga na msikiti na kuimarisha uhusiano wao. Mkuu wa kila kaya anawajibu wa kuimarisha uhusiano wake na misikiti na kuwazoesha ahali zake pia ili kizazi chetu kiwe imara kwenye imani na itikadi zetu na kujaaliwa na baraka tele za kiungu. Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kuelewa vyema majukumu yetu na kuyatekeleza ipasavyo. Aamina



Maneno ya Busara

"Ni afadhali kuwa na jeshi la kondoo linaloongozwa na Simba, kuliko jeshi la simba linaloongozwa na kondoo."-

Napoleon_Bonaparte.

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*



Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad[ra] Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

MKATABA BAINA YA WAHAAJIR NA MA ANSWAR NA WAYAHUDI

mbali na kuwafanya Waislamu kuwa ndugu, Mtume[saw] alitengeneza mkataba kwa ajili ya watu wote wa Madina. Aliwakusanya viongozi wa Wayahudi na wa Waarabu na kusema:

"Awali, hapa, kulikuwa na makundi mawili tu, lakini sasa kumekuwa na makundi matatu, yaani mwanzoni hapa walikuwa wakiishi tu Wayahudi na Waarabu wa Madina, lakini sasa yamekuwepo makundi matatu ya Wayahudi, Waarabu wa Madina na Wahamiaji kutoka Makka. Hivyo kunapaswa kuwepo na mkataba wa amani kati yetu."

Hivyo pamoja na makubaliano ya pamoja, ukaandikwa pia mkataba fulani. Maneno ya mkataba huo ni haya:

'Mkataba baina ya Mtume wa Allah, Muhammad[saw], Waaminio na watu wote wale wanaokubali kwa ridhaa na furaha kuuingia. Kama yeyote auawe miongoni mwa Wahamiaji, basi wao wenyewe (wahaajir) ndio watakaohusika (kuhusiana na kifo chake). Jukumu la kuwaachisha huru wafungwa wao litakuwa ni lao wenyewe. Na kwa namna hii hii, makabila mbalimbali ya Waislamu wa Madina nayo pia yatabeba yenyewe majukumu ya mambo haya. Yeyote atakayeeneza uasi au kuanzisha uadui au kuleta mfarakano ndani ya nidhamu, basi wote waliofanya mkataba watasimama dhidi yake, hata kama awe ni mwanawe. Kama kafiri auawe na mwislamu vitani, basi Waislamu wenye undugu na yule aliyeuawa hawatalipa kisasi dhidi ya mwislamu na wala kafiri wa aina hiyo hatasaidiwa kupambana na mwislamu. Sisi sote tutamsaidia Myahudi yule atakayeungana nasi (katika mkataba huu). Wayahudi hawatapewa usumbufu wa aina yoyote na adui yeyote yule hatasaidiwa dhidi yao. Yeyote asiyekuwa mwaminio hatawapa watu wa Makka hifadhi ndani ya nyumba yake na wala hataweka amana za mali zao na wala hatajiingiza kwa namna yoyote ile ndani ya mapambano kati ya Makafiri na Waaminio. Kama mtu yeyote amtendee vibaya mwislamu bila ya sababu yoyote, basi Waislamu wote watafanya juhudi ya pamoja dhidi yake. Kama adui mshirikina aishambulie Madina basi Wayahudi watashirikiana na Waislamu na kuchangia gharama za vita. Makabila ya Wayahudi yaliyokwisha fanya mapatano na makabila mengine ya Madina watakuwa na haki kama zile walizo nazo Waislamu. Wayahudi watabaki na dini yao na Waislamu watabaki na dini yao. Haki watakazopewa Wayahudi, haki hizo hizo watapewa pia wanaowafuata. Miongoni mwa watu wa Madina, hakuna yeyote atakayeweza kuanzisha vita bila ya ruhusa ya Mtume wa Allah, Muhammad[saw] Lakini chini ya sharti hili, hakuna mtu yeyote atakayezuiwa kujilipizia kisasi kinachostahiki. Wayahudi watabeba wenyewe gharama za kuendesha Tandhim yao na Waislamu pia watabeba wenyewe gharama za kuendesha Tandhim yao. Lakini katika sura ya vita wote watashirikiana. Madina itakuwa ni sehemu yenye kuheshimika kwa watu wote waliomo ndani ya mkataba huu. Watu wageni wanaokuja chini ya himaya ya wenyeji wa mji, watatendewa kama vile wanavyotendewa wenyeji. Lakini watu wa Madina hawatakuwa na ruhusa hii ya kumuweka mwanamke yeyote majumbani mwao bila ya ruhusa ya familia ya mwanamke huyo. Magomvi na fujo vitapelekwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kwa ajili ya kutolewa maamuzi. Washiriki wa makubaliano haya hawataingia katika mapatano yoyote na watu wa Makka au washirika wao. Hii ni kwa sababu washiriki wa mkataba huu, wanakubaliana katika kupigana na maadui zao kwa pamoja. Washiriki wa makubaliano haya wataungana katika amani kama vile katika vita. Hakuna atakayeingia katika amani ya peke yake. Lakini hakuna atakayelazimishwa kushiriki vita ya mwenzake. Hata hivyo, mshiriki atakayepita kiasi katika vita kwa namna yoyote ile atastahili adhabu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Ndiye Mlinzi wa watu wema na Waaminio na Muhammad ni Mtume Wake (Hisham).

Huu ndio muhtasari wa mkataba. Ndani ya mkataba huu imesisitizwa mara kwa mara kwamba uaminifu na utakaso hautaachwa asilan na mdhalimu atawajibika mwenyewe kwa udhalimu wake. Ni dhahiri kutokana na mkataba huu kwamba uamuzi huu ulikuwa umeshafanywa na Mtume[saw] kwamba Wayahudi na wenyeji wa Madina wasiokuwa waislamu watatendewa kwa huba, upendo na huruma na watafanywa kama ndugu. Hivyo magomvi yote yaliyotokea baadae na wayahudi yalisababishwa kikamilifu na wayahudi wenyewe.

Itaendelea toleo lijalo

Hae! Msiba Mzito

Na **Mahmood Hamsin Mubiru**

Siku ile ya ahadi,
Aloipanga Wadudi,
Ameitika Rashidi,
Wito wa Mola Jalia.

Mja atarudi kwangu,
'Kupokea lake fungu'
Hiyo mipango ya Mungu,
Rashidi kaitikia.

Kaitika pasi shaka,
Mwito wa Mola Rabuka,
Huo mwito wa baraka,
Mikono tunainua.

Chini ya chake kivuli,
Vyote vilivyo jamali,
Mpatie ya Jalali,
Tuli apate tulia.

Nipo kwenye pembe yangu ninayoipenda Masjid Salaam. Kitabu nilicho nacho mkononi kimekwishanitoa hapa nilipo na kunipeleka mbali. Nikiwa huko baidi, nasikia sauti; Assalaam Alaikum. Naitikia Waaleyikumsalaam. Naweka kitabu chini. Ni kijana wangu Rashidi Mbega huku akitabasamu ananieleza; "Mzee nataka kujifunza Kiingereza". Namtazama huku nami nikitabasamu; *"Acha masihara Rashidi", "Kiingereza gani tena nikufundishe, Kiingereza chako mbona kizuri tu"*. Hapana, anasisitiza. Nami namwambia wewe unachokihitaji ni kujiendeleza zaidi. Nakupa njia. Nitakuwa ninakupa riwaya nzuri za Kiingereza. Hiyo moja ninayokupa isome kwa makini. Andika maneno usiyoyajua. Sentensi tamu ambazo uzikumbuke kwa ghaibu. Tutapata nafasi ya kuyazungumza hayo maneno magumu. Tukakubaliana Inshallah kesho nitamletea riwaya moja na akimaliza hiyo nitamletea nyingine.

Tukio hilo sitalisahau na ndiyo lililojenga ukaribu na kijana huyu na nikawa ninamheshimu. Hivyo ilikuwa ni huzuni kubwa tarehe 01/08/2022 nilipopata habari za kufariki kwa Rashidi Juma Mbega. Rashidi Mbega alizikwa tarehe 02/08/2022 kwenye makaburi ya Jamaat yaliyopo Wailes Temeke. Sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Kwa tukio hilo nilijifunza mambo mawili matatu. Mapenzi ya kupenda kusoma ambayo yanaonekana kupotea katika jamii yetu. Pili ni jambo la busara kujua kuwa hujui na hivyo kujitahidi kujua. Rashidi ingawaje alikuwa anajua Kiingereza aliona bado achukue hatua ya kujiendeleza zaidi. Huyo aliyekuwa antaka kujifunza Kiingereza alikuwa mwalimu mzuri wa Kiingereza huko mitaani! Hilo linabaki kuwa somo kwetu sote.

Mapenzi ya kuwapa wengine lile alilokuwa anajua yalikuwa makubwa. Vijana wengi amewafundisha Kiingereza na hata elimu hiyo ya umeme wa jua (Solar energy) amewapatia wengi. Hakuwa na uchoyo katika kutoa elimu. Ni sifa nyingine nzuri ya kuigwa.

Kipaji hicho na uwezo aliokuwa nao vyote hivyo amevitumia vizuri katika kuendeleza miradi ya Jamaat. Kwa moyo mkunjufu alifanya kazi za kusambaza umeme wa jua (Solar energy) sio hapa tu nchini bali pia huko Uganda. Huko nchini Uganda ameacha sifa kubwa ya kijana aliyependa na kuthamini shughuli za dini. Watu wa Uganda walifurahia sana kazi aliyoifanya kiasi hiki ya kwamba Mhandisi Ali Kamaga sahib ambaye walifanya kazi naye huko Uganda alipopata habari za kifo chake alifunga safari ya kuja kuhudhuria msiba. Siku zote alizokuwa Dar es salaam zilikuwa ni za majonzi na huku akidondokwa na machozi. Amir sahib nchini Uganda ameandika barua ya kutoa pole kwa Amir Tanzania na timu nzima ya waliyokuwa wakifanya kazi ya umeme wa jua (Solar energy) hapa nchini. Katika barua hiyo Amir sahib na Mbashiri Mkuu nchini Uganda Mh. Muhammad Ali Kaire sahib anaandika;

Ndugu wapendwa,
Yah: Barua ya rambirambi:
Kwa niaba ya Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya nchini Uganda, Ofisi ya Amir na Mbashiri Mkuu imesikitishwa sana kusikia kifo cha bw. Rashidi Mbega mtumishi aliyejitolea sana chini ya shirika la IAAAE –U.K
Jamaat Ahmadiyya Uganda inawapa

Inaendelea uk. 5

Hae! Msiba Mzito

Kutoka uk. 4

pole wafanyakazi wote wa IAAAE duniani kote, familia yake na Jamaat ya Tanzania kwa ujumla. Sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Wanajamaat wa Ahmadiyya nchini Uganda wana uhakika kwamba kifo cha Rashidi Mbega kimeleta majonzi makubwa kwa kumpoteza mtu muhimu kwa shirika la IAAAE, familia yake na marafiki. Hatuna maneno ya kutosha ya kueleza msiba huu. Tunachoweza kufanya ni kuendelea kumuombea kwa Allah kwamba roho yake ipate amani ya kudumu. Mwenyezi Mungu Aweze kumsamehe mahali popote ambapo aliweza kuteleza na Ampatatie nafasi peponi. Ameen.

Licha ya barua hii ya rambirambi Mwenyekiti wa IAAAE nchni Uganda tayari yupo njiani kuelekea Tanzania kwenye mazishi hayo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Awape ustahmilivu na uvumilivu katika kipindi hiki kigumu.

Wassalaam,

Wenu ***Muhammad Ali Kaire***

Amir na Mbashiri Mkuu

Ahmadiyya Muslim Association – Uganda.

Sawa na tulivyoshuhudia na kama barua hiyo kutoka kwa Amir sahib na Mbashiri Mkuu wa Jamaat Ahmadiyya Uganda ilivyoeleza, Rashidi Mbega hakusita wala kupepesa macho pindi alipoitwa kufanya kazi ya Jamaat. Kila alipoitwa aliitika na kuwa tayari kutumika. Kipaji alichopewa cha kufahamu mambo kilikuwa kikubwa na mapenzi yake ya kuendelea kutafuta kwenye mitandano na vitabu kulimuongezea umahiri wa kujua vitu vingi. Nakumbuka nikiwa na Abdillah Kombo alitueleza kwa muda mrefu sayansi ya mazoezi ya mwili na faida zake. Kila hatua ya mazoezi alieleza kwa nini.

Na tumekuja kuelewa baadaye ya kwamba alihakikisha kwamba vifaa vyote vya kazi zake alikuwa navyo na hivyo vilimuwezesha kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Vifaa hivyo vilikuwa vingi kiasi hiki kwamba kwenye sanduku lake vikiwekwa vilikuwa havibebeki bila kupata usafiri maalum.

Wakati tunamkumbuka Rashidi ni jambo la muhimu kumkumbuka na kumuombea baba yake Mzee Juma Mbega sahib ambaye alikuwa ni Mwanajamaat madhubuti ambaye pamoja na Mzee Saidi Mzee Muharram sahib walitumikia Jamaat na kwa mapenzi makubwa walikuwa wanamletea Sheikh Muhammad Munawwar Amir na Mbashiri Mkuu baadhi ya bidhaa ambazo kwa wakati ule zilikuwa hazipatikani kwa urahisi nchini. Wanajamaat hao walikuwa ni madereva wa malori ya kwenda nje ya nchi. Bila shaka Rashidi alipata malezi mazuri kutoka kwa baba yake na kutoka utotoni alikuwa na mfungamano na Msikiti.

Sote tunafahamu mtihani wa fedha unavyomkabili binadamu. Ukichanganya na hali ngumu ya maisha tunayopitia kwa hivi sasa. Hayo yote hayakuwa kizingiti kwa Rashidi Mbega ambaye alifanikiwa kutoa michango yake yote ya Wasia. Mwalimu Yusuf Mwishehe ananiambia kwamba Rashidi alikuwa mwanachama wa Wasia na alikuwa analipa michango yake kwa wakati na hakuwa na deni idara ya wasia imeeleza.

Juma Msalizi Kazema alinieleza kwamba siku za hivi karibuni Rashidi alikuwa ametoa mchango wake kwa ajili ya jengo la Tanzim ya Ansarullah linaloendeela kule Kitonga. Rashidi alikuwa ametoa ahadi ya kushughulikia suala zima la umeme katika jengo hilo.

Kilicho chako hasa ni kile ulichokitanguliza na hicho ndicho utakachokikuta huko tuendako. Moja ya alama ya mwaminio ni 'Wamimmaa Razaqnaahum yunfikuun' (Na hutoa katika vile walivyoruzukiwa –Kurani Tukufu).

Dalili nyingine ya malezi mazuri aliyoyapata ni wakati wa ugonjwa wake huu wa mwisho. Ndugu yake wa karibu alitaharuki na kuanza kuleta mambo ya ushirikina. Rashidi alikasirika sana kiasi hiki ya kwamba asifike kumuona. Akiwa anakuja arudie kule. Jitihada zilifanyika za kuwapatanisha na ndugu yake lakini Rashidi alikataa kata kata akieleza uchafu unaotokana na ushirikina. Alikuwa anakwenda hospitali na la msingi alikuwa anamuandikia Huzoor (atba) kwa ajili ya maombi. Kitu gani tena kingine alichokuwa anahitaji? Alama nyinigne ya imani thabiti.

Rashidi alijijengea utamaduni wa kumuandikia barua Huzoor kwa kila hatua aliyochukua katika maisha yake. Barua nyingi za majibu yake kutoka kwa Huzoor (atba) zilikuja wakati akiwa kitandaninahivyohakupatabahati ya kuzisoma. Wale waliomuuguza siku za mwisho wanakumbuka jambo moja muhimu ambalo ni vigumu kulisahau. Katika hali ya maumivu kugeuka huku na huku Rashidi neno lake lilikuwa ni moja tu 'Alhamdulillah'

Lipo la kujifunza kwa sisi ambao hatujaamka katika hilo la kuwa na mawasiliano na Huzoor (atba).

Wakati nafanya utafiti kuhusu makala haya. Mwalimu Yusuf Mwishehe alinieleza kuwa siku moja kabla ya kifo cha Rashidi alimuona katika njozi kuwa Rashidi ni mwenye kutabasamu na mwenye hali nzuri mno. Na mwalimu alishangaa sana kuwa huyu bwana si mgonjwa mbona yupo kwenye hali nzuri na mwenye furaha tele? Asubuhi yake ndipo alipopata habari za kifo chake.

Nafsi iliyofaulu ni ile inayojitayarisha kwa ajili ya safari ile. Hakuna anayejua siku ya kutoka kama anavyokumbusha Shaabani Robert;

Siku ya mauti kuja, mtu hana kimbilio
Kuja budi itakuja, kama si kesho ni leo
Kila mtu humfuja, pasi ya mapendeleo
Habaki mtu mmoja, katika safari hiyo

Tunakuomba yailahi, sote utupe safari njema.

Abdul Majid Katangulia

Na **Mwandishi Wetu**

Historia ya ujenzi wa msikiti wa Songea kwa mapana na marefu haiwezi kukamilika bila kutaja tena kwa heshima familia mbili za Farouk na Varda na katika kutaja familia hizo utakuwa umekosea sana bila kumtaja kinara wao Abdul Majid Farouk, aliyetutoka siku ya Idi 10.7.2022 Hospitali ya Taifa Muhimbili na kuzikwa jioni ya siku hiyo makaburi ya Jumuiya ya Ahmadiyya Temeke, Sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Bwana Abdul Majid Farouk alisimama kidete na imara katika ujenzi wa msikiti wa Songea. Sheikh Muhammad Munawwar, Sheikh Zabih na Sheikh Rafiq Malik walitoa shukurani maalum za ushujaa wa bwana Abdul Majid kwa jinsi ambavyo hakupata lepe la usingizi hadi msikiti wa Songea umesimama. Abdul Masjid alikuwa kiungo kizuri cha familia mbili za Farouk na Varda.

Ushujaa huu na uimara wa Abdul Majid unatokana na malezi ya baba yake bwana Farouk ambaye yeye alijiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya siku za mwanzoni mwanzoni wakati wa Sheikh Mubarak Ahmad. Ukoo wa Farouk kwa Mapenzi makubwa ulishiriki katika ujenzi wa msikiti wa Songea. Mabinti wawili wa Abdul Ghani Farouq ambao ni wazazi wa Abdul Majid, Yunus (senior), Rafiq, Ibrahim, Aziz, Iqbal, Yunus (Junior). Mabinti hawa wa bwana Farouk walitoa mapambo yao ya thamani na kuyauza ili kuendeleza ujenzi wa nyumba ya Allah. Na hadithi ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. inasema atakayemjengea Allah nyumba hapa duniani nay eye atamjengea nyumba peponi. Ni alama ya Uchamungu wa hali ya juu kwani Allah Anasema *Hamtaufikia wema hasa hadi mtoe katika vile mnavyovipenda*.

Bwana Abdul Majid hakupumzika hata kidogo. Ikumbukwe siku hizo zilikuwa ngumu sana. Vitu vilikuwa adimu na vinapatikana kwa kibali. Majid alipigakambi ofisi ya Mkuu wa Mkoa na hakutoka hadi alipopata kibali cha kununua mabati. Lawrence Gana, Mkuu wa Mkoa siku hizo alitoa kibali na Majidi alikwenda moja kwa moja hadi dukani, akanunua bati na kuziweka kwenye mkokoteni hadi ulipokuwa unajengwa msikiti. Ni Mapenzi makubwa ambayo yalimfanya msimamizi wa msikiti huo kumuandikia barua Abdul Majid tarehe 13/06/1984 "Kazi hii ya ujenzi nilipoanza, wewe na Varda family mlikuwa wasaidizi wangu wakubwa na jambo hili siwezi kusahau mimi wala wanajumuiya wa Songea."

Moja ya Ushahidi wa ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ni uwezo kwa msaada wa Allah kuanzisha Jamaat ambayo imeondoa kabisa mipaka bandia ya Jiografia na rangi na kujenga undugu kuliko hata ule wa yule mliyetoka tumbo moja. Mapenzi yaliyokuwepo baina ya Abdul majid na Athuman Ndembo yalikuwa ya aina na yaliacha gumzo. Msingi wake ni wote kumkubali Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. Ilikuwa muhali kwa watu wawili hawa kushinda bila kuonana. Athumani Ndembo akienda dukani kwa Abdul Majid Farouk wataanza kuzungumza mambo ya kiroho na kusahau wateja waliokuja kununua vitu dukani.

Akiwa Songea, Iringa na Dar es salaam, Abdul majid farouk aliendelea kuwa na mfungamano na msikiti. Yeye na vijana wake wawili hawakukosa msikitini siku ya Ijumaa. Katika mazungumzo yetu niligundua ni mtu ambaye alipenda sana kusoma vitabu na elimu yake juu ya Jamaat ilikuwa kubwa. Abdul Majid Farouk ametuachia mifano miwili inayongára. Kujitolea katika njia ya Allha na kudumisha mfungamano na msikiti. Na wameahidiwa yaliyo mema wale wenye mfungamano na msikiti.

Bustani ya Washairi

AHMADIYYA NA MAENDELEO YA KISWAHILI – TANZANIA

Na **Mahmood Hamsin Mubiru**

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

Kurani Tukufu kwa Kiswahili.

106. Kafasiri taratibu,
Tena kwa kubwa adabu,
Ni maneno ya Wahabu,
Aliyeumba dunia.

107. Kwa Kiswahili shufaka,
Kitabu akakiweka,
Sheikh wetu Mubaraka,
Rabi Alituletea.

108. Ni kiswahili bayana,
Ni kiswahili mwanana,
Ni kiswahili safina,
Chombo cha kutuvushia.

109. Watu walitaajabu,
Kazi ile mahabubu,
Ya kufasiri kitabu,
Alicholeta Jalia.

110. Ni Kuruani tukufu,
Aliyoleta Lutufu,
Akatupa msahafu,
Kwa kiswahili ajaa.

111. Milango ikafunguka,
Watu wakachangamka,
Ikawa inasomeka,
Kwa roho zilotulia.

112. Kumbe inawezekana,
Kuifasiri bayana,
Kwa hino lugha mwanana,
Mola alotupatia.

113. Ujinga ukatoweka,
Nuru ikatuzunguka,
Kwa maneno ya Rabana,
Tukawa twazingatia.

114. Huo haukuwa mwisho,
Msambe ni hitimisho,
Ila ni mwanzo wa mwisho,
Vingine katuletea.

Zawadi ya Maulidi.

115. Zawadi ya Maulidi,
Maisha yake Seyidi,
Tumwa wetu Muhammadi[saw]
Macho akatufungua.

116. Kwa lugha ilo nyepesi,
Katueleza unasi,
Ipi ni yake nafasi,
Mtume wetu Nabia.

117. Muhammad muujiza,
Maishaye katujuza,
Ona alivyotimiza,
Alotumwa kutwambia.

118. Kazaliwa ni yatima,
Pagumu mbele na nyuma,
Ila kaishi kwa wema,
Kwa adabu na murua.

119. Kabla ya kuzaliwa,
Mtume wetu Rasuwa,
Baba yake alikuwa,
Tayari katangulia.

120. Mama mzazi Amina,
Na yeye walitengana,
Sita angali kijana,
Umri wake Rasua.

121. Hakuwa na ukorofi,
Hata na huo ulafi,
Na kelele za makofi,
Yeye hakukaribia.

122. Michezo ya kipuuzi,
Hakushiriki azizi,
Jambo hili liko wazi,
Mabaya aliambaa.

123. Kakuwa kawa kijana,
Mwenye huluka mwanana,
Hata walo na hazina,
Zao walimuachia.

124. Akiwa Al amini,
Watu wakamuamini,
Akaziweka nyumbani,
Mali akawatunzia.

125. Lakabu yake Sadiki,
Alisemalo la haki,
Hakuwa na uzandiki,
Na maneno ya kuzua.

126. Palikuwa na maneno,
Ya kuleta utengano,
Nani ataleta lino,
Jiwe hili la usia.

127. Na wote walikubali,
Atayefika awali,
Nyumba hino ya Jalali,
Jiwe atatuwekea.

128. Mara kaja Muhammad[saw]
Wote wakaona sudi,
Huyu mtu wa Wadudi,
Jibu atatupatia.

129. Kilemba akakiweka,
Viongozi kawataka,
Kubeba hadi kufika,
Mahala palo sawia.

130. Hapo yeye alishika,
Sawasawa kaliweka,
Wote walifurahika,
Ni sawa bini sawia.

Mama wa waaminio

131. Habari zikaenea,
Kila pembe kusambaa,
Hadija kazisikia,
Mama huyo wa ulua.

132. Mti unajulikana,
Matunda utayaona,
Tena ya kila namna
Mtini kujichumia.

133. Mama aliyesifika,
Utajiri kadhalika,
Katika mji wa Maka,
Sifaze zilienea.

134. Binti Huwailadi,
Katika yake fuadi,
Karidhika Muhammad[saw],
Waweze kufunga ndoa.

135. Kaongoza msafara,
Kwa hekima na busara,
Shahidi ni Marisara,
Kwa Hadija katongoa.

136. Kaeleza kwa makini,
Mwenendo wake amini,
Kama ua la uzani,
Sifa kummiminia.

137. Hadija akapeleka,
Ujumbe ukamfika,
Nikahi ikafungika,
Pasipo na kuchelea.

Utaendelea toleo Lijalo

MBEGA AMETANGULIA.

1. Twasema innalillahi, ilaihi rajiuna.
Tumetoka kwa ilahi, kwake tutarudi tena.
Kwa kifo kisositahi, yeyote kumtafuna.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

2. Twajihisi tumezihi, Mbega hatutamuona.
Mwana jamati salihi, mwema asiyejivuna.
Hakuwa mtu kabihi, leo hatunaye tena.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

3. Alikuwa mubalighi, dini kahubiri sana.
Ali na siha sahihi, na mwenye jisimu pana.
Hakuwa mtu wa fihi, uchoyo aliukana.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

4. Kama nyota ya mirihi, aling'ara huyu bwana
Kamwe hakuzikirihi, amuri za Maulana.
Alinogesha wajihi, wa jamati ya Rabana.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

5. Na alikuwa fasihi, wa kutenda na kunena.
Mpole kisha mcheshi, siye wa kununa nuna.
Kamwe hakuwa mshashi, tangu akiwa kijana.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

6. Ufundi alikubuhi, umeme na zake zana.
Kwa ya dini masilahi, alijitolea sana.
Hakutaka sitizahi, kwenye mambo ya maana.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

7. Alifikwa na maradhi, makali yakambana.
Matabibu wafawidhi, kiume wakapambana.
Na ponyo halikukidhi, kwa matakwa yako Bwana.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

8. Umemwita ya Ilahi, ambaye tulipendana.
Basi mpe masilahi, mema na yaliyonona.
Mtunze umsitahi, katika pepo mwanana.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

9. Nasi nduguze wa ruhi, twakuomba Sub hana.
Mwenza wake wa nikahi, aliyebaki na wana.
Rabi wape islahi, uwashushie sakina.
Moyo waniuma sana, Mbega ametangulia.

10. Kwa sala na tasbihi, usiku hata mchana.
Mola tunakusabihi, kaziyo kosa haina.
Mbega tutamsabahi, akhera tukionana.
Moyo waniuma sana. Mbega ametangulia.

Abdullah H. Mbanga (KUNGWI)
Radio Ahmadiyya 99.3, Mtwara.
Kungwi@gmail.com

WE HABIL JIHADHARI

1. Bismihi Rabbina, Allah Mola Azizi
Ndiye wetu Maulana, Muumbaji na mlezi
Swadu aso na Mwana, simzawa si mzazi
We Habil Jihadhari, Kain hana Simile

2. Swallu alanabiyina, Sharafu ya wakufunzi
Muhammad Sayidina, Allahu chake kipenzi
Wasalamu Alayna, Sisi waja wa Mwenyezi
We Habil jihadhari, Kain hana simile

3. Ndungu Zangu waugwana, Namnasihi Habili
Maasum huyu Mwana, Mja aso ufedhuli
Mtabadi wakina, Yazimiye kwa jalali
We Habil Jihadhari, Kain hana simile

4. Makini kaku hatari, UsfehijA azali
Umwena leo ya kheri, Umri ufike mbali
Tuase kwa mistari, Na njema zako amali
We Habil Jihadahari, Kain hana simile

5. Likitotoma kw asana, Giza usake kulunzi
Panapo lugha gongana, Aga nenda kabarizi
Amani utai sana, Wazi pasi na kengezi
We Habil jihadhari, Kain hana simile

6. We Habil jihadhari, Epusha shari kamili
Twajua Hana kiburi, Siji nadi ukisali
Kitoa sadaka nzuri, Fumbata sijingobel
We Habil jihadhari, Kain hana simile

7. Zi japo jema shauri, Dadavua kwa akili
Usima kwa jeuri, Usikike kwa akali
Ongea kisiri siri, Kipayuka utafeli
We Habil jihadhari, Kain hana simile

8. Nuhuri kwa tusubiri, Twende muda kiwasili
Kimchokora jasiri, Huna salama Habili
Uinga mue Hatari, Sijechinjwa kikatili
We Habili jihadhari, Kain hana simile.

Mwl Muhammad Habibu

MKE NA MUME (MUME NIRUHUSU)

Mke.
Mfalume muadhwamu, songa hapa mume wangu,
Ni muda myezi shatimu, simuoni mama yangu,
Nami moyo unahamu, niruhusu mume wangu,
Niruhusu mume wangu, nende kwetu kutembea.

MUME.
Laazizi akiramu, kipenzi changu mwajuma,
Jawabu lako naamu, hakuna kwenda kwa mama,
Walkathiri fahamu, baki ndani mahashuma,
Hakuna kwenda kipenzi, baki ndani laazizi.

MKE.
Habibi switi azizi, mume ninae kupenda,
Una wivu siku hizi, siwezi kuja kutenda,
Nimewapeza wazazi, nipa ruhusa kuenda,
Niruhusu mume wangu, nende kwetu kutembea.

MUME.
Switi hati laazizi, hakuna kwenu kuenda,
Natunza langu penzi, yaniwajibu kulinda,
Kuna mangi siku hizi, mabaya sije kuganda,
Hakuna kwenda kipenzi, baki ndani laazizi.

MKE.
Habibi itowe khofu, hakuna wakuniiba,
Nitafanya wadilifu, pamwa kumukhofu RABA,
Natamani kuwashufu, mama na mwenziwe baba,
Niruhusu mume wangu, nende kwetu kutembea.

MUME.
Sikhofu uwaminifu, nakwamini mahabuba,
Imani sasa dhwaifu, wakora watakukaba,
Si pesa wala mikufu, vyote vivyo wataiba,
Hakuna kwenda kipenzi, baki ndani laazizi.

MKE.
Sahihi wala sipingi, mtaa mevurugika,
Waovu sasa ni wengi, kote wametawanyika,
Baba mbona steringi, mtaani asifika,
Niruhusu mume wangu, wezi wananiogopa.

MUME.
Huwezi kwenda mwajuma, mume leo nimefunga,
Bakia upike nyama, pamwe na kukanda unga,
Kesho panapo uzima, safari tutaifunga,
Usijali laazizi, kesho tutaenda wote.

MKE.
Namshkuru RAHIMA, muumba mbingu na anga,
Alo nipa mume mwema, mpaka leo naringa,
Senendi tena kwa mama, ngoja nikakande unga,
Nimekwelewa lazizi, kesho pia nayo siku.

SoMo De Prìñçê Tz.
Tanga, Tanzania

SALAMU KWA IMAM

Salamu mpendwa wetu, upole Kwa majukumu
Kuihudumu jamatu, Hakika ni kazi ngumu
Akupe mema jannatu, muumba wetu rahimu
Amiri wetu imamu, furaha yetu ikwako

Amiri wetu imamu, furaha yetu ikwako
Uwepo wako imamu, salama Dunia Iko
Twamshukuru karimu, maamuma nyuma yako
Siha njema kupatie, bariki maisha yako.

Masihi Omary Stambuli Kisagwa

PUMZIKA KWA AMANI ABASI A. KASITA

Na **Harun Rashid Bundala**

Shauku ya kusoma Mapenzi ya Mungu, Safina ya Nuhu na Quran Tukufu aliyopewa na Dokta vyote hivi vilimsukuma Bwana Abasi Abdallah Kasita kupata shauku ya kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya, Jumuiya aliyoendelea kuienzi na kuitumikia hadi siku yake ya mwisho alipopata ajali tarehe 29/04/2022 na kufariki. Sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Maisha ya Kasita yametawaliwa na Shauku ya kutafuta elimu. Mwaka 1945 hadi 1959 alipomaliza masomo ya sekondari ilikuwa ni miaka ya kutafuta elimu. Ni Mapenzi hayo ya kusoma yaliyomuongoza kwenye njia iliyonyooka na hatimaye kujiunga na Ahmadiyya mwaka 1956.

Kuzingatia kwake sala na malezi ya watoto ni sifa ambazo ametuachia ukiwa mfano mkubwa. Wakati anapata ajali alikuwa akielekea kwenye sala ya Ijumaa.



Ni sifa hizo zilizofanya apate fursa ya kutumikia Jamaat katika uwanja wa uongozi. Amewahi kuwa Rais wa Mkoa wa Tabora na Nazim Ála katika Tanzim ya Ansarullah. Kwa msaada mkubwa wa Allah kwa kipindi chake chote alikuwa ni kiongzi wa vitendo sio maneno. Alitoa michango yake na kusimamisha sala. Mapenzi yake kwa Jamaat Ahmadiyya yalikuwa makubwa kiasi hiki ya kwamba mwaka 1057 kilipoanzishwa chou cha kwanza cha wabashiri kilichokuwa kinaongozwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi na Mwalim wa Kiingereza akiwa Mwalim B.K. Heri. Bwana Kasita alimtuma mdogo wake kwenye chou hicho ili awe Mubashir wa dini ya Islam.

Mazishi ya mpendwa wetu Abasi Abdallah Kasita aliyezaliwa tarehe 10/05/1935 yalifanyika tarehe 01/05/2022 kijijini alikozaliwa Mbalanga wilaya ya Igalula na kuongozwa na Maulana Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya.

Nenda mwenzetu we nenda, pumzika kwa Amani
Akulinde kwa kupenda, Muumba wetu Manani
Tusiwekwe njia panda, tuwekwe kwenye hisani
Nenda tutakukumbuka, kwa baraka za Manani

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

NIKAH	DHIAFAT	UNAJIMU	TABIBU
IKHLAS	TANBIHI	URUHUBANI	KURUNZI
IHLAM	ZIRAAT	ISLAMABAD	HADUBINI
KHILAFAT	KIKOKOTOZI	MARKAZ	DARUBINI
MAHDI	TAWHIID	MULAQAT	ISTIGHFAR
WAQFEEN	TANZIA	MUADHAM	
UTANDAWAZI	MDAHALO	MHANDISI	
TADHKIRAH	UPAGANI	MAULANA	

J	Z	I	Z	Z	T	L	J	I	N	A	G	A	P	U	I	C	P	T
T	X	N	K	P	T	T	G	M	H	R	T	G	V	N	Z	I	C	J
B	I	I	J	M	M	C	N	N	A	H	N	A	I	M	H	N	L	N
R	S	B	U	A	Z	B	Q	R	K	J	A	B	W	I	N	L	Q	N
G	T	U	M	H	T	T	R	G	I	V	U	R	B	H	W	M	M	M
T	I	D	I	D	A	N	R	Y	N	R	L	N	I	Y	I	A	C	U
A	G	A	J	I	F	I	H	L	A	M	A	M	C	K	U	I	H	L
N	H	H	A	M	A	R	Z	D	K	T	U	M	A	L	H	R	D	A
Z	F	X	N	L	I	M	T	O	T	H	D	B	A	R	I	D	L	Q
I	A	C	U	X	H	N	M	W	T	A	I	N	I	N	K	G	A	A
A	R	B	J	L	D	M	T	T	H	O	A	L	A	B	W	A	D	T
Z	I	Z	A	W	A	D	N	A	T	U	K	B	A	A	A	P	Z	M
M	W	M	N	L	B	N	L	V	N	T	U	O	Q	F	N	T	U	I
T	F	V	L	H	L	O	M	F	R	H	S	F	K	N	A	A	B	Z
D	P	Z	I	R	A	A	T	K	U	A	E	J	X	I	D	T	B	N
I	S	I	D	N	A	H	M	R	L	E	Q	P	B	H	K	M	N	U
X	N	M	T	N	N	T	U	H	N	P	N	M	A	T	L	L	Z	R
K	C	M	R	N	H	F	K	X	V	C	R	M	P	N	Q	H	P	U
K	T	R	X	K	X	I	S	L	A	M	A	B	A	D	V	Y	F	K

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.





Jinsi ya kupika Chapati za Maji

Na **Mtandao [Facebook: JinsiYaKupika]**



MAHITAJI

1. Ngano ½ kilo
2. Mayai 3
3. Mafuta ¼ kikombe

kitunguu kikubwa kilichosagwa 1

4. Kitunguu Swaumu punje 4
5. Chumvi ½ kijiko au zaidi kulingana na matakwa yako

JINSI YA KUPIKA

1. Chekecha unga wako vizuri weka katika bakuli safi.
2. Tia maji katika bakuli la unga na ukoroge mpaka upate uji wa wastani si mzito sana wala si mwepesi sana.
3. Ongeza mayai na chumvi endelea kukoroga.
4. Ongeza kitunguu swaumu na kitunguu maji. Injika kikaango chako jikoni subiri kipate moto.
5. Chota pawa moja mimina na tandaza kuzunguka kikaango subiri sekunde tano hadi kumi mpaka ikauke kisha geuza upande wa pili.
6. Tia mafuta huku ukigeuza na kuzungusha ili mafuta yaenee pande zote na ili chapati isiungue. Endelea kugeuza mpaka iwe rangi ya kahawia.
7. Hapo chapati zitakua tayari kwa kuliwa Fanya hivyo kwa chapati zote zilizobakia.

KUTOKA MAKTABA

Na Ally Hamisi Mbambwa

Sardar Nazeer Ahmad Sahib

Meli ilirudi Bandarini

Alikuwa katikati ya Shuguli ya mahubiri. Aya na Hadithi zikimtoka akieleza na akiwafafanulia maswala mbalimbali ya kufika kwa Masih Aliyeahidia a.s. Waarabu wa nchi ya Aden. (Yemen). Mahubiri yalinoga hasa. kutahamaki, jioni imeingia! Akatoka mbio hadi Bandarini, Akakuta Hola, Meli imemuacha!. Laa haulaa!

Walimcheka na kumdhihaki vya kutosha wale aliokuwa anawahubiria. Hakika Alifadhaika sana. Alifadhaika kwa kuachwa na meli akiwa mtu Muhimu kabisa katika meli hiyo. Bali, La hashaa! Hakufadhaika kwa masimango juu ya ujumbe aliowafikishia.

Aliondoka kwa unyonge na kutafuta sehemu ya kuupitisha usiku akiwa hajui la kufanya, sababu Meli hiyo ilikuwa sio ya kurudi leo wala kesho, ikiondoka ndio imeondoka.

Sardar Nazeer Ahmad Sahib, alikuwa ni Daian ila-llah mwenye shauku na mapenzi makubwa ya kuhubiri. Alipokuwa akiingia kwenye kazi ya kuhubiri, alikuwa anasahau kila kitu.

Yeye mwenyewe anahadithia kuwa; "nilikuwa nimeajiriwa kama Daktari katika meli iliyokuwa ikibeba mahujaji wakati wa Hija. Safari fulani wakati tunarudi nyumbani baada ya Hajji, meli ilipiga nanga kwenye bandari ya Aden. Nilishuka na kuingia mitaani kuhubiri, nikamezwa kabisa katika shughuli hii kiasi ya kwamba nikasahau kabisa muda wa meli yetu kuondoka. Baada ya mahubiri niliporudi bandarini, La haula!, meli imeshaondoka kitambo. Hakika nilifadhaika sana. Nilijiuliza, viongozi wangu watanifikiriaje kuhusiana na hili.

Iwapo Hujaji yeyote atafariki kwenye Meli, bila shaka nitawajibika kisheria kutokana na uzembe wangu.

Watu niliokuwa nakiwahubiria walinidhihaki na kunicheka kwamba meli yangu imekwenda na sasa nilikuwa kwenye matatizo makubwa. Nilipitisha usiku mzima nikimuomba Allah kwamba, "*Ee Allah, nilikuwa nikitekeleza kazi yako ya kufikisha ujumbe kwa waarabu. Hii haikuwa kazi yangu binafsi. Sasa meli imeondoka sijui la kufanya. Ee Allah nakuomba uirudishe meli hiyo*". Wakati nikiwaza hayo yote, nilipitiwa na usingizi. Nilipata ndoto. Katika ndoto niliona Meli imerudi.

Asubuhi nilipotangaza kwamba Mungu wangu Amenijulisha kwamba meli imerudi, watu walizidi kunidhihaki na kunicheka sana. Lakini nani awezaye kuhukumu maajabu ya Allah. Yeye Ana uwezo usio na kikomo na njia zake ni za ajabu.

Asubuhi kulipopambazuka, watu walijionea tamasha la ajabu. Mtu mmoja alikuja mbiombio na kunifahamisha kwamba, kweli meli ilikuwa imeingia bandarini. Nilimshukuru Allah na kuanguka kumsujudia na kisha nilikwenda moja kwa moja kwenye meli.

****

*Tukifanya kazi za Allah, Allah Hupokea maombi yetu kwa haraka sana na hutusaidia.

Itaendelea Inshallah

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA*as*

Dhambi - ambayo kusema kweli ni sumu - hupatikana pale mtu akosapo utiifu kwa Mwenyezi Mungu na anapokuwa na utovu wa upendo Wake na kumbukumbu Yake yenye shauku. Hakika ya mtu ambaye moyo wake umeganda dhidi ya mapenzi ya Mungu ni sawa na mti uliong'olewa na hauwezi tena kunyonya lishe ya uzima toka ardhini. Katika hali kama hiyo pole pole mti hunyauka na kufa, hivyo chambiliche kukauka kwa mti, dhambi huusibu moyo. Tiba za ukavu huu, sawa na kanuni za maumbiIe, ni za aina tatu:

(I) Upendo, (2) Istighfar, yaani kumwomba Allah msamaha. Kiuzungumzi, hii ina maana ya kutamani kuzika au kufunika, ikimkumbusha mtu ya kwamba mradi mzizi wa mti umezikika ardhini lipo tumaini la mti kuota tena majani mapya. (3) Tiba ya tatu ndiyo tauba (toba) hii ikiwa na maana ya kumgeukia Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu kujivutia lishe ya uzima, na mtu kujisogeza karibu naye zaidi, na kujichubua kwa msaada wa matendo mema gamba la madhambi alilo nalo. Toba haipatikani kwa maneno matupu ya mdomo; kusema kweli, toba yaweza tu kukamilika kwa msaada wa matendo ya kitawa. Matendo yote ya wema yana lengo la kufikia ukamilifu wa toba.

(Roohani Khazain Jal. 12, UK. 328: Sirajuddin Isai ke char Sawalon ka Jawab Uk. 2-3)

MATUKIO KATIKA PICHA





Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akifanya mazungumzo na viongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania wakiongozwa na kaimu Amiri wa Jumuiya hiyo Sheikh Abdulrahaman Ame, mazungumzo yaliofanyika Ikulu Jijini Dar es salaam tarehe 15 Agosti 2022.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania mara baada ya mazungumzo yaliofanyika Ikulu Jijini Dar es salaam tarehe 15 Agosti 2022.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango akiagana na kaimu Amiri wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Tanzania Sheikh Abdulrahaman Ame, mara baada ya mazungumzo yaliofanyika Ikulu Jijini Dar es salaam tarehe 15 Agosti 2022.

Muharram

Kutoka uk. 1

huu, jitahidini sana kumsalia Mtume[saw] kwani Mtume[saw] ndiye aliyetufundisha siri hii kwa ajili ya kukubaliwa kwa maombi na mpenzi wake wa dhati (Masihi aliyeahidiwa[as]) alituelekeza makhsusi kwenye jambo hili kwa kutuelezea baraka za sala ya Mtume[saw] kwa kitendo. Lakini daima mkumbuke kwamba kwa kumsalia Mtume[saw], mnapaswa kujinyanua hadi daraja lile ambapo sala ya Mtume[saw] humsaidia mtu. Ikiwa mnamsalia Mtume[saw], basi mnapaswa kutambua cheo chake pia."

"Wazao wa kimwili wa Mtume[saw] ambao walidumisha uhusiano wao wa kiroho naye, bila shaka wanastahili mapenzi yetu na wanastahili sana."

Hadhrat Maihe Ma`ud[as] alisema kuhusu Hadhrat Imam Husain[ra]" Husain[ra] alikuwa safi na mtukufu na bila shaka yu miongoni mwa wale waja watukufu ambao Mwenyezi Mungu Huwatakasa kwa mkono Wake Mwenyewe na kuwajalia mapenzi Yake. Bila shaka yeye ni miongoni mwa viongozi wa peponi na kuwa na bughudha dhidi yake sawa na chembe kunaweza kumfutia mtu imani yake. Taqwa yake, mapenzi yake ya Mungu, subira, uimara, uchamungu na ibada ni mfano mwema kwetu. Umeangamia moyo unaomchukia na umefaulu moyo unaodhihirisha mapenzi yake kwa kitendo" (Majmua Ishteharat, Jal 3, Uk,545)

Basi haya ndiyo mapenzi ambayo kila mwahmadiyya anatakiwa awe nayo kwa Hadhrat Imam Husain[ra]ambayo ametufundisha Hadhrat Masihe Ma`ud[as].

Kadhalika tunayo heshima katika nyoyo zetu kwa Masahaba pia, tunayo heshima katika nyoyo zetu kwa Hadhrat Abu Bakr[ra], Hadhrat Uthman[ra], na Hadhrat Umr[ra]. Siyo kwamba tukipenda upande mmoja, mapenzi ya upande mwingine yanapungua. Tunatakiwa tuwapende wampendao Mwenyezi Mungu na Mtume Wake[saw].

Akieleza hadhi ya masahaba, Hadhrat Masihe Ma`ud[as] alisema " Masahaba watukufu walionyesha uaminifu ule katika njia ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake mpaka walisikia sauti isemayo رضی اللہ عنھم و رضوا عنہ. Hiyo ndiyo hadhi ya hali ya juu waliyojaliwa masahaba yaani *Mwenyezi Mungu Aliwaridhia nao walimridhia Mungu*" (Malfudhat, Jal, 4, Uku,465)

Hivyo basi tunawapenda sana wapendwa wote wa Mtume[saw]. Mwenyezi Mungu Aujalie umati wa kiislamu uweze kumaliza mfarakano wa kila aina kwa sababu upinzani wa nje nao umeshika kasi siku hizi. Leo tuna haja ya kuinama mbele ya Mungu tukiwa pamoja. Sasa vita inayoendelea baina ya Israeli na Palestina, wapelestina wadhulumiwa wanapata hasara kubwa kutokana na kukosa mwongozo sahihi,wanajitia hasara wenyewe. Katika zama hizi Hadhrat Masihe Ma`ud[as] alisha toa mwongozo kwamba msipigane vita kwa jina la dini, vita yoyote itakayopiganwa kwa jina la dini, hamtaishinda. Tena vita hiyo haina uwiano wowote, akili ya mtu inadai kwamba tatizo hili litatuliwe kwa mazungumzo ili kuokoa maisha ya watu wasio na hatia" (Khutba Juma, Jan,2, 2009)

Sikilizeni yaa Uli-Albabi

Na Ramadhan Kagobe
Magomeni Mikumi

ULI-ALBABI, ni watu wenye kutumia akili wakati wote. Iwe anafanya jambo la kimwili au la kiroho matumizi ya akili kwake ni Aula. Na mtu anapoacha kutumia akili basi huyu anakuwa kishapotea njia anapokwenda hapajui na alipotoka hapakumbuki.

Na ndio maana katika Kurani Allah Karim Ametilia mkazo sana matumizi ya akili, kiasi kwamba bila ya kutumia bongo barabara huwezi nasema abadan, asilan ukayajua maneno ya Allah na Mtume wake. Ni kupitia mlango wa akili unaweza kumuelewa Subhana Wata'ala. Bila shaka tuna yakini kabisa na kadari za Allah zipo, humuongoza amtakae vile apendavyo. Aya za kutilia mkazo jambo hili ni nyingi mno – mpaka sehemu moja ndani ya Kurani Mungu Anasema wazi wazi kabisa – na nina hakika aya hii ni Muhkam – haina songi-songi – yaani haina kona kona katika kuielewa. Inasema hivi; Hakika wanyama wabaya zaidi mbele ya Allah ni viziwi mabubu ambao hawatumii akili. (Al Anfal:23). Mtu aachapo kutumia akili ipasavyo sawa na ilivyokadiriwa na Allah anapoteza thamani yake kabisa na kuwa duni kuliko viumbe vyote. Na ndio maana Mungu Akasema huyu mtu anakuwa ni mnyama mbaya kabisa. Tunafahamu kwa yakini viumbe vingine vyote havina akili vinaishi kwa hisia tu, na ndio maana unaoana hakuna mabadiliko yoyote katika maisha yao.

Ng'ombe atabaki hivyo hivyo alivyo siku zote hali kadhalika wanyama wengine wote. Maendeleo ya nchi za magharibi zote wao kuwa mbele sana katika maisha ya kidunia – sababu kuu ni hiyo hiyo kwamba wenzetu matumizi ya akili katika shughuli zao ni kubwa – isitoshe wana jitihada isiyopimika. Mfano kama ni kilimo watajitahidi kufanya utafiti juu ya zao analotaka kulima – afahamu ni hali ipi inayofaa katika zao analotarajia kulima, maji, madawa na kadhalika. Anapoanza kulima analimma kweli kweli na matokeo yanakuwa ni ya kuridhisha. Wakati mwingine matokeo yanakuwa si ya kuridhisha, wao huwa wanafuatilia kwa makini sana na kufahamu kwa uhakika kwa nini matokeo yamekuwa mabaya. kwa neno zima matumizi ya akili yana nafasi kubwa sana.

Hii habari ya kilimo ni mfano tu, ilivyo ni kwmaba katika mambo yao yote wafanyayo matumizi ya akili yapo juu sana – ikifuatiwa na jitihada. Sasa kwa upande wetu – kwa mfano hapa kwetu Tanzania tunalima-lima – lakini sehemu kubwa ya wakulima wetu ni wa kawaida sana, hakuna utafiti ubora wa mbegu – hata hali ya ardhi kulinganisha na zao unalolima hujui. Na matokeo yake mara nyingi yanakuwa ni duni sana. Pindi matokeo yanapokuwa hivi huyoo anakwenda kwa mganga wa kienyeji amjulishe kwa nii hali imekuwa hivyo. Mganga naye anamjulisha kuwa ni jirani yako ndio amefanya hivi. Masikini! Mara mkulima na jirani yake wanagombana sana na wakati mwingine wanafikia hatua ya kupoteza maisha. Lakini ukitizama chanzo cha matatizo yote haya ni matumizi madogo ya akili. Kwa sababu matumizi ya akili ni kidogo basi tumefungua miliango ya ushirikina katika maisha yetu, kiasi hiki kwamba ushirikina imekuwa ni sehemu ya imani.

Sehemu nyingine katika Kurani inasema hivi; Je Mnawaamuru watu kutenda wema na mnajisahau nafsi zenu hali mnasoma kitabu Je hamtumii akili? (2:45). Unaona jinsi mwanadamu alivyo anapoacha kutumia akili yake, basi uwezo wake wte unapotea kiasi kwamba anakuwa hata yeye mwenyewe hajui. Sawa na aya - isemavyo unawaamuru wengine wawe watu wema – wakati wewe unayafanya hayo hayo. Mfano, unawafahamisha jamaa msiwe wezi, wewe mwenyewe unaiba, usizini mwenyewe unazini, usiwe muongo mwenyewe kidhabi dhabina – kwa kuwa hutumii akili – hata ile hali ya kujiona au kujijua kwamba unakosea inapotea kabisa. Hivi ndivyo hali ya mwanandam inakuwa pindi anapoacha kutumia akili yake.

Na maisha ya dunia hii si kitu ila mchezo na upuuzi na bila shaka nyumba ya akhera ni bora zaidi kwa wale wamchao (Allah), basi je hamtumii akili? Iwapo mtu atatafakari kwa makini ni hakika iliyo wazi na dhahiri kwamba maisha ya dunia hii ni upuuzi unapolinganisha na maisha ya akhera.

Kwanza maisha ya dunia hii ni mafupi sana. Ndugu zetu, jamaa zetu wengi waliotangulia mbele ya Allah walikuwa na kati ya miaka 60 mpaka 70. Wapo waliowahi kufariki mapema chini ya miaka hiyo, na wapo waliopata umri mrefu zaidi ya miaka 80 na kuzidia hapo. Isipokuwa wengi wametawafu wakiwa katika miaka ya 60 hadi 70.

Na hata wale ambao wanapewa umri mrefu huwa ni taabu tu, maradhi yanakuwa mengi kama vile kisukari, shinikizo la damu, kuishiwa nguvu kwa ujumla, macho kupoteza uwezo wa kuona, wakati mwingine hata uwezo wa akili unaanza kupungua. Kwa hiyo basi maana halisi ya maisha huwa inatoweka kabisa. Mtu ambaye akili yake ni timamu kabisa hawezi kujitaabisha sana na maisha haya ya dunia na akapuuzia akhera yake. Kwa sababu ana yakini kwamba hapa yupo kwa muda mfupi sana. Hatupingi mtu kuwa na maisha bora na mazuri, hii imehimizwa hata ndani ya Kurani kwamba pindi tumalizapo kusali, basi tuendelee na kazi zetu kama desturi. Pia ipo hadithi ya Mtume s.a.w. inayosema kuwa tushughulike na maisha ya dunia kana kwamba hatutaondoka kesho. Watu wa Ulaya na Amerika wao wamechukua nusu tu ya maelezo ya hadithi kwa kuamua kujishughulisha kwa nguvu zote juu ya maisha ya dunia – akili zao zote, nguvu zao zote, na jitihada zote katika dunia na kwa kweli wamefanikiwa sana, kama tunavyoona maendeleo yao – lakini upande wa pili wako chini sana, kwa sababu upande huu wa maisha ya akhera hawapo kabisa – na matokeo yake ni kama tuyaonavyo wamekwenda chini sana kiasi ambacho wanamfanya binadamu kama wao kuwa ni Mungu, wanamuabudu na kumtii kama Mungu wao. Baadhi ya dini zao zinahalalisha ushoga, mwanaume amuoe mwanaume mwenziye, mwanamke anaoa mwanamke mwenziye. Hali zote hizi wamefikia ni pale tu walipoacha kutumia akili ipasavyo.

Baadhi ya wakati inastaajabisha sana kuona watu wa magharibi ni weupe mno upande wa kiroho ukilinganisha na maendeleo ya kimwili au ya kidunia waliyonayo. Tulitarajia kwamba wao walistahili kuwa mbele zaaidi kutokana na uelewa wao juu ya maisha ya kawaida. Kwa hiyo basi, ilivyo hasa mwanadamu hana namna yoyote ya kuishi bila ya matumiz ya akili. Moja ya njia ya kukuza uwezo wa akili ya mwanadamu ni usomaji wa vitabu. Tujitahidi sana kusoma vitabu vya aina mbalimbali kuanzia Quran, vitabu vya Masihi, vitabu vya Hadithi za Mtume s.a.w. na hata vitabu vya watu wa kawaida. Tunapokuwa ni wavivu katika matumizi ya akili zetu na akili pia inaanza kuchoka na kuchakaa, hii ni kanuni ya maumbile, kitu chochote ambacho kimeumbwa kwa ajili ya kazi fulani kisipotumika kwa lengo lake lililokussudiwa huharibika.

Sasa hata akili zetu iwapo tutakuwa hatutumii akili zetu mara kwa mara ipasavyo itafikia mahali tutashindwa kujua kitu chochote. Kujiuliza mara kwa mara, kutafakari mambo, kuuliza ni mambo pia yanasaidia uimara wa akili. Mfano mwingine mimi kwetu ninakotoka idadi ya Waahmadiyya ni chache sana, mara nyingi nimekuwa nikijiuliza hivi ni kwa nini hali imekuwa hivi? Jitihada za mahubiri zimefanyika kwa muda mrefu, tena na watu alimu pia wachamungu waliokuwa wakifanya kazi hiyo, lakini wapi! Sasa mimi binafsi nikaamua nifanye utafiti kidogo kw akuwa nawauliza baadhi ya watu maswali, kwamba kwa nini haumkubali Masihi wa Mtume s.a.w. – baadhi ya majibu Muhindi hawezi kuwa Nabii, huyu bwana alifia mahala pabaya sana, wengine walisema iwapo angesema yeye ni Sheikh ningekubali, lakini kuwa yeye ni Mtume hapo sikubali.

Waliompinga Nabii Isa a.s. wao walimuomba ageuze milima ya mawe iwe mikate. Na waliokuwa wakimpinga Mtume s.a.w. wao akili yao yote ilizama katika mali na kumtaka apande mbinguni kisha aje na dhahabu mkononi, halafu awe na bustani ambayo mto wa maji unatiririka ndani yake.

Itaendelea toleo Lijalo

JALSA SALANA TANZANIA
2022

Amir na Mbashiri Mkuu nchini anapenda kuwaarifu Wanajumuiya wote kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili tarehe 30 Septemba, 1 na 2 Oktoba 2022, katika eneo la Jumuiya, Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah.

JALSA SALANA TANZANIA MUBARAK

Jalsa Salana Uingereza 2022

Kutoka uk. 12

unaoweka na kuhifadhi haki za wanawake katika maana halisi.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kuwa mtu mmoja kutoka ofisi ya Uhamiaji nchini Kongo-Kinshasa alijiunga na Jumuiya alipokuwa akitazama matukio ya Jalsa Salana. Baada ya kusikiliza hotuba ya Hadhrat Khalifatul Masih*atba*, alianza kushangaa kwa nini yeye hakuwa tayari Mwahmadiyya na akaapa kuja mara nyingi zaidi na kufanya utafiti zaidi.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba mwanamke wa Kialbania alisema kwamba baada ya kutazama Jalsa atazingatia kwa dhati ukweli wa Ahmadiyya na akasema kwamba baada ya kusikiliza hotuba za Hudhur*atba*, aligundua kwamba anakubaliana na yale anayoyasema Hudhur*atba*.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba mwanamke mmoja mwenye asili ya Afghanistan alisema kwamba alipata amani kubwa baada ya kumsikia Hudhur*atba* na kujifunza namna Uislamu unavyolinda haki za wanadamu. Alisema hiyo ilimfurahisha sana, kwani nchini Afghanistan, chini ya utawala wa Taliban, wanawake hawana thamani yoyote. Hata hivyo, alijifunza namna ambavyo Uislamu unaweka na kushikilia haki za wanawake.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba kulikuwa na marafiki wawili kutoka Guyana ya Ufaransa waliosema kwamba siku mbili kabla ya Jalsa, walikuwa wakizungumza kuhusu jambo hili kuwa je Uislamu una mafundisho yoyote kuhusu haki za wanadamu. Kisha walipotazama Jalsa Salana na kusikiza hotuba ya Hudhur*atba* kwa wanawake, basi walishangazwa mno kwa kujua jinsi Uislamu unavyosimamia haki za wanawake.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* aliwasilisha hisia za mwanajumuiya mpya wa kike kutoka Afrika aliyesema kwamba baada ya kusikiliza hotuba za Hudhur*atba*, ni wazi kwamba hatupaswi kuwa Waahmadiyya ili tu kuwaongoza wengine kwa Ahmadiyya, bali lazima tujirekebishe kwanza ili watu katika jamii waione sura halisi ya Uislamu kupitia mienendo yetu mema, na lazima maneno na matendo yetu yalingane. Hudhur*atba* alisema kwamba kwa kawaida watu husema kwamba Waafrika hawajasoma, lakini mwanamke huyu kutoka Afrika amegundua kitu ambacho hata wasomi wa Ulaya hawajaweza kutambua. Kwa hivyo, yafaa watafakari sana juu ya jambo hili.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba mwanajumuiya mpya kutoka Kazakhstan alisema kwamba maneno ya Hudhur*atba* yalikuwa na athari kubwa kwake yeye na mke wake nao walikaa pamoja na kutazama matukio yote ya Jalsa. Pia aliwaombea wale waliojitolea kufanikisha mipango yote ya Jalsa Salana.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba mzee wa miaka 80 kutoka Zambia hakuweza kuzuia machozi yake wakati wa hotuba ya Hadhrat Khalifatul Masih*atba* na hata ilimbidi kuondoka nje, kwani alikuwa amepatwa na jazba. Baadaye, alieleza kwamba hii ilikuwa mara yake ya kwanza kusikia sauti ya Khalifa, jambo lililomfanya apatwe na jazba sana. Baadaye, aliwaeleza wanajumuiya kwamba kazi ya kujaza msikiti na Waahmadiyya haipaswi kuachiwa wabashiri tu, bali kila mtu lazima ajitahidi kutekeleza jukumu hili.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba mwalimu wa historia kutoka Albania alisema kwamba ingawa alihudhuria Jalsa hivi majuzi, lakini alihisi kana kwamba alikuwepo kwenye Jalsa. Alisema kwamba Jalsa hii ilikuwa ni ushahidi tosha kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya imeungana na iko tayari kumsikiliza Khalifa wa Ahmadiyya na kutii maneno yake. Alisema kwamba hotuba za Hudhur*atba* zilikuwa rahisi kueleweka kwa watu wote na yafaa tufuate mawaidha yake.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kuwa kuna tofauti ya masaa manane na nusu kati ya London na Adelaide, Australia. Mbashiri wa Adelaide alisema kwamba alikuwa na wasiwasi kama watu wataweza kuja kutazama Jalsa, kwani itakuwa usiku sana kwao. Hata hivyo, wanajumuiya walionyesha ikhlasi kubwa na walikuja usiku kutazama mipango ya Jalsa na hata walikaa hadi saa tisa asubuhi kutazama hotuba ya mwisho ya Jalsa Salana iliyotolewa na Hudhur*atba*.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba mwanamke mmoja Mwarabu aliandika kwamba alishukuru sana kujifunza kwamba anafuata dini inayomhifadhi na kulinda haki za wanawake kwa kiwango hicho. Alisema kwamba anajisikia fahari kufikisha mafundisho haya ya Uislamu kwa marafiki zake. Alisema kwamba Hudhur*atba* pia alivutiwa na mkazo juu ya jinsi wanawake wanavyopaswa kutoa haki za wanaume, na amekuwa akichambua jinsi anavyoweza kufanya hivyo vyema zaidi kwa baba yake, kaka na mume wake.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kuwa mwanajumuiya mpya kutoka Malaysia hakuwa na pesa za kutosha kulipia malipo ya mtandao na kutazama matukio ya Jalsa. Kwa hiyo, alichukua baadhi ya maembe kutoka kwenye mti nje ya nyumba yake, akayauza, na kisha kwa pesa hizo, alinunua data ya kutosha ya mtandao ili kuweza kutazama mwenendo wa Jalsa.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba mwanamke mmoja kutoka Guinea-Bissau alisema kwamba alikuwa na mashaka mbalimbali kuhusu Uislamu, hata hivyo mashaka haya yote yaliondolewa aliposikiliza hotuba ya kumalizia ya Hudhur*atba* na kisha akatangaza kujiunga na Uislamu Ahmadiyya. Alisema kuwa katika siku na zama hizi za leo, Ukhalifa ndio unatoa majibu ya masuala ya ulimwengu wote.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba mtu mmoja kutoka Albania alisikiliza hotuba za Hudhur*atba* katika Jalsa na akasema kwamba zilikuwa zimejaa Aya za Qur'ani Tukufu na matukio ya maisha ya Mtume Mtukufu (s.a.w). Baada ya kwenda nyumbani, alipiga simu na kusema kwamba alikuwa amesoma masharti kumi ya bai'at na akaamua kujiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya.

Jinsi Taarifa Za Matukio Za Jalsa Salana Zlivyowafikia Mamilioni Ya Watu Duniani:

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* kwamba jumbe 126 zilipokelewa kutoka kwa viongozi wa serikali wa sehemu mbalimbali za dunia. Nchi 53 zilijiunga na Jalsa kupitia video kutoka duniani kote. BBC, ITV, Metro na vyombo vingine vya habari viliangazia Jalsa Salana, huku tovuti nane zenye kufikia jumla ya watu milioni 20 pia zilichapisha makala kuhusu Jalsa. Katika vyombo vya habari vya magazeti, makala 14 kuhusu Jalsa yalichapishwa, na wasomaji milioni 1.2. Jalsa Salana ilitangazwa katika vipindi 32 vya TV na watazamaji zaidi ya milioni 12 wakatazama. Jalsa Salana ilitajwa katika vipindi 33 tofauti vya redio vyenye wasikilizaji zaidi ya milioni 1. Watu mbalimbali walichapisha kwenye mitandao ya kijamii kuhusu Jalsa ambao idadi yao ilikuwa zaidi ya milioni 12.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kuwa video na picha za MTA zilifikia zaidi ya watu milioni 4. MTA Africa inaripoti kuwa Jalsa Salana ilionyeshwa kwenye vituo 20 vya TV barani Afrika, na kuwafikia watu milioni 35.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kuwa Jarida la Review of Religions pia lilisambaza taarifa za Jalsa kupitia mitandao ya kijamii na YouTube. Nakala 40 zilichapishwa, video 12 zilitengenezwa na zaidi ya machapisho 110 ya mitandao ya kijamii yalifikia watu 300,000.

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba hii ilikuwa ni mifano michache tu aliyoitoa. Hudhur*atba* aliomba kwamba athari za Jalsa ziweze kudumu milele.

Sala Ya Jeneza:

Hadhrat Khalifatul Masih*atba* alisema kwamba ataongoza sala ya jeneza ya wanajumuiya waliofariki wafuatao:

Bi. Nusrat Sultana Qudrat Sahiba:

Bi. Nusrat Sultana Qudrat Sahiba wa Canada, mke wa Qudratullah Adnan Sahib. Alikuwa akisimamisha sala na alikuwa na tabia za kimalaika. Akiwa hospitalini, hapakuwa na daktari ambaye hakueneza kwake ujumbe wa Uislamu. Kulikuwa na daktari Mwislamu ambaye alikuja kumwona na kumsikiliza akisoma Kurani Tukufu. Alikuwa na mapenzi makubwa kwa Ukhalifa. Ameacha mumewe na wanawe watatu, akiwemo Raziullah Noman, mwanafunzi wa Jamia Ahmadiyya Canada. Mumewe anasema kwamba aliishi maisha yake kama mtu anayejitolea wakfu maishani. Alikuwa na shauku sana ya kufanya ubashiri na akawafunza sana watoto wake tabia hiyo ambao pia wana shauku ya ajabu ya ubashiri, hasa mwanawe Raziullah Noman. Hudhur*atba* alimwomba Mwenyezi Mungu amwezeshe yeye na ndugu zake daima kuendeleza urithi huu wa mama yao. Hudhur*atba* alimwomba Mwenyezi Mungu Ainyanyue daraja yake Peponi.

Bw. Chaudhary Latif Ahmad Sahib:

Chaudhary Latif Ahmad Sahib alifariki hivi karibuni. Alikuwa amejitolea wakfu maisha yake na aliwahi kuwa Naib Wakilul Mal Thani na Naib Wakilul Mal Thalith. Alihudumu pia barani Afrika. Miaka ya huduma zake kwa jumla ni zaidi ya nusu ya maisha yake. Alikuwa mnyofu sana na mwenye kujali hisia za watu na aliwatendea kwa wema wale wote waliofanya kazi naye. Hudhur*atba* amesema kuwa ameacha nyuma mwana mmoja na binti mmoja, na akamwomba Mwenyezi Mungu Amjaalie maghfirah na rehema na Ainyanyue daraja yake Peponi.

Bw. Mushtaq Ahmad Alam Sahib:

Mushtaq Ahmad Alam Sahib wa Kashmir. Ameacha mke, wana sita na binti wawili. Wanawe watatu ni wabashiri, mmoja wao anatumikia Jumuyia nchini Senegal na hakuweza kuhudhuria mazishi ya baba yake. Hudhur*atba* aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Awape subira na pia Akaomba kuwa marehemu ajaaliwe kupata daraja ya juu Peponi.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

MUHAR.-SAF.1444AH | SEPTEMBA 2022 | IKHA 1401 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu[saw]

Imesimuliwa na Hadhrat Ibn Umar[ra] ya kuwa: Mtume[saw] alisema: "Msijihusishe katika mazungumzo mengi isipokuwa yanayohusika na kumkumbuka Allah. Maana kuzungumza sana bila ya kumtaja Allah huufanya moyo kuwa mgumu! Na mtu aliye mbali sana na Allah ni mwenye moyo mgumu" (**Tirmidh**)

Jalsa Salana Uingereza 2022

Baraka, Shukrani na Maombi

Baraka Na Athari Za Jalsa Salana:

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 12/08/2022; baada ya kusoma Tashahhud, Tawwudh na Surah Al Fatiha Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano[atba] alisema kwamba sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu kwamba Alituwezesha kufanya Jalsa Salana, Uingereza mwaka uliopita na mwaka huu pia, na baraka nyingi zilishuhudiwa katika siku hizi tatu.

Kushinda Vikwazo Vya Corona katika Maandalizi ya Jalsa Salana:

Hadhrat Khalifatul Masih[atba] alisema kwamba hapo awali ilifikiriwa kuwa labda Jalsa italazimika kufanywa kwa kiwango kidogo kwa sababu ya janga la corona. Hata hivyo, mwezi mmoja kabla, iliamuliwa kuwaruhusu Waislamu Waahmadiyya wanaoishi nchini Uingereza. Awali wasimamizi walikuwa na wasiwasi jinsi ambavyo Jalsa ingeweza kufanyika, hata hivyo ilifanyika kwa mafanikio na baraka nyingi.

Hadhrat Khalifatul Masih[atba] alisema kwamba Jalsa inatazamiwa kwa hamu sana, na inapofika mwisho, inapita haraka sana kiasi hiki kwamba hata mtu hajitambui. Kulikuwa na watu mbalimbali waliositasita kuhudhuria Jalsa kutokana na maradhi ya corona na sababu nyinginezo. Hata hivyo, wanajumuiya walikuwa wakimwomba Mwenyezi Mungu, na Hudhur[atba] akasema kwamba alikuwa akiomba vile vile, na kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu, Jalsa iliendelea vizuri.

Jitihada za Kutochoka za Watu wa Kujitolea katika Utekelezaji wa Majukumu yao:

Hadhrat Khalifatul Masih[atba] aliwashukuru wale wote waliojitolea kutoa huduma mbalimbali kwa bidii sana tangu mwanzo hadi mwisho. Vijana au wazee, wanaume au wanawake, kila mtu alifanya kazi kwa juhudi kubwa na kwa bidii. Kuna mapungufu kadhaa ambayo hujitokeza, hata hivyo, haya yote ni mambo yanayoweza kuboreshwa kwa siku zijazo. Kwa ujumla, kila mtu alitoa haki ipasavyo kutolewa kuhusiana na wajibu wake na Hudhur[atba] aliwashukuru hao wote.

Hadhrat Khalifatul Masih[atba] alisema kuwa MTA ilifanya kazi nzuri ya kuonyesha taarifa za matukio. Mwaka huu, walijenga studio nzima wenyewe iliyowasaidia kuokoa maelfu ya pauni. Waliweza kuungana na nchi mbalimbali duniani walioweza kuonana, huku kila mmoja akitazama Jalsa. Hudhur[atba] aliishukuru MTA kwa kuuonyesha ulimwengu umoja wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya na kuwanyamazisha wapinzani.

Athari Nzuri Sana ya Jalsa Salana kwa Watu Wanaoishi Kote Duniani:

Hadhrat Khalifatul Masih[atba] aliwasilisha matukio mbalimbali kutoka duniani kote ya wale waliopata athari nzuri sana ya mipango ya Jalsa Salana. Mtu mmoja asiyekuwa Mwahmadiyya kutoka Niger alionyesha mshangao wake juu ya kiwango cha utii na umoja chini ya Khilafate Ahmadiyya, na jinsi kila mtu alivyokaa kimya kusikiliza hotuba za Hudhur[atba].

Hadhrat Khalifatul Masih[atba] alisema kwamba Mwislamu mwingine asiyekuwa Mwahmadiyya kutoka Burkina Faso alitazama mwenendo wa Jalsa Salana na akalazimika kusema kwamba hakika huu ni Uislamu wa kweli. Mwislamu mwingine asiyekuwa Mwahmadiyya kutoka Syria alisema kwamba wameitazama Jalsa na juhudi zilizofanywa kueneza ujumbe wa kweli wa Uislamu duniani kote, atasoma zaidi kuihusu Jumuiya Ahmadiyya.

Hadhrat Khalifatul Masih[atba] alisema kuwa mtu mmoja kutoka Guine-Konakri alikuwa akiona nchi zote mbalimbali zikionyeshwa kwenye luninga walipokuwa wakitazama Jalsa, hata hivyo, hakuona Guine-Konakri. Mara tu alipofikiria hili, picha kutoka Guine-Konakri zilionyeshwa kwenye luninga. Pia alielezea shukrani zake kwa hotuba iliyotolewa na Hudhur[atba] kuhusu haki za wanadamu.

Hadhrat Khalifatul Masih[atba] alieleza hisia za mwanajumuiya kutoka Zambia, aliyesema kwamba awali alifikiri kwamba Uislamu ulinyima haki za wanawake. Hata hivyo, baada ya kusikiliza Hotuba ya Hadhrat Khalifatul Masih[atba] kuhusu haki za wanadamu, alitambua kwamba badala ya Ukristo, ni Uislamu ndio

Endelea uk 11

KITABU KIPYA



Nidhamu Mpya

Katika hali ya nyuma ya itikadi zilizokuwepo za ukomunisti na demokrasia ya kibepari, mrithi wa pili wa Jumuiya ya Ahmadiyya, Hadrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad[ra], alihutubia mhadhara huu kwenye Mkutano wa Mwaka wa Ahmadiyya tarehe 28 Desemba 1942. Hotuba hiyo inajibu swali, *'Je, Ahmadiyyat, Uislamu wa Kweli, unapendekeza vipi kushughulikia tatizo kubwa la kukosekana kwa usawa wa kijamii na kiuchumi duniani?'* Suluhu la Ahmadiyya ni suluhisho la Uislamu lililoundwa chini ya mwongozo wa Mungu kwa mahitaji ya sasa na Waasisi Watakatifu wa Jumuiya ya Ahmadiyya.

mzungumzaji huchunguza na kuchambua dhima iliyochezwa na tofauti

harakati za kupunguza umaskini na mateso, kama vile, Ujamaa, Ujamaa wa Kimataifa, Umaksi, Ubolshevim, Unazi na Ufashisti na kadhalika. msemaji pia, anachunguza dini kuu za ulimwengu kuhusu swali la msingi 'kutokuwa na usawa wa kijamii ni tatizo zito.'

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi[as], mwanzilishi wa Ahmadiyya Muslim Jama'at, aliweka misingi ya Mpango Mpya wa Dunia, kwa kuanzisha mpango wa Wasiyyat yenye msingi wa mafundisho ya Kiislamu na chini ya mwongozo wa Mwenyezi Mungu katika kitabu chake Al-Wasiyyat kilichoandikwa mwaka 1905. Baadaye mwaka 1934 Hadrat Mirza.

Bashiruddin Mahmud Ahmadra alizindua Tahrik-e-Jadid ili kuandaa mazingira ya utekelezaji kamili wa Mpango Mpya wa Ulimwengu wa taasisi ya Wasiyyat. Katika mhadhara huu wa sasa anafafanua malengo na malengo ya Tahrik-e-Jadid na anadai kwamba Mfumo Mpya wa Ulimwengu katika nyanja zake zote, kiuchumi, kijamii na kidini, kama ilivyoletwa na Nizam-e-Wasiyyat, mwishowe utashinda na mapinduzi mapya na ya kweli yatafanyika.

Jipatie nakala yako kwa bei ya Tsh 3,400/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com